25 JUNI, 2013

# BUNGE LA TANZANIA

---

# MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA KUMI NA MOJA

**Kikao cha Hamsini na Sita - Tarehe 25 Juni, 2013**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Naibu Spika (Mhe. Job Y. Ndugai) Alisoma Dua*

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati Ifuatazo Iliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:-**

Taarifa ya Mwaka na Hesabu Zilizokaguliwa za *TCRA Consumer Consultative Council (TCRA (CCC)* kwa Mwaka ulioshia tarehe 30 Juni, 2012 *(The Annual Report and Audited Accounts of TCRA Consumer Consultative Council (TCRA – CCC) for the Year Ended 30th June, 2012).*

**MASWALI NA MAJIBU**

Na. 457

**Wakuu wa Mikoa/Wilaya Kuwa Wabunge**

**MHE. CHRISTOWAJA G. MTINDA** aliuliza:-

Moja ya majukumu ya Bunge ni kuisimamia na kuishauri Serikali na pia Ibara ya 67(2)(g) ya Katiba ya Jamhuri

ya Muungano wa Tanzania inaeleza kukoma kwa mtu kuwa Mbunge endapo mtu huyo amepewa madaraka ya Afisa Mwandamizi katika Utumishi wa Umma.

(a) Je, ni kwa maana gani Wabunge ambao ni Wakuu wa Mikoa au Wakuu wa Wilaya wanatimiza majukumu yao ya Kibunge?

(b) Je, ni kwa namna gani viongozi hao wanakiuka Ibara ya 67(2)(g)ya Katiba pamoja na kuwa wanateuliwa na Rais?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, URATIBU NA BUNGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Christowaja Gerson Mtinda, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, Wabunge ambao ni Wakuu wa Mikoa au Wilaya wanatimiza majukumu yao ya Kibunge kwa kuzingatia Ibara 63(3)(a) – (e) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wabunge ambao ni Wakuu wa Mikoa na Wilaya hawakiuki Ibara ya 67(2)(g) ya Katiba kama ilivyonukuliwa na Mheshimiwa Mbunge. Ibara hiyo inafafanua kuwa mtu anaweza poteza sifa za kuwa Mbunge iwapo ameshika madaraka ya Afisa Mwandamizi katika Utumishi wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano isipokuwa madaraka ambayo Rais anaweza au anatakiwa kukabidhi kwa Mbunge kwa mujibu wa Katiba au Sheria iliyotungwa na Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, Katiba iliyopo inampa Mheshimiwa Rais mamlaka ya kuteua Watanzania wenye sifa kuwa Wakuu wa Mikoa au Wilaya wakiwemo Waheshimiwa Wabunge. Hata hivyo hoja ya kutenganisha majukumu ya mihimili yetu ya dola imejitokeza pia katika

mapendekezo yaliyowasilishwa na wadau kwenye Tume ya Mabadiliko ya Katiba. Hivyo basi ni matumaini ya Serikali kwamba uamuzi kuhusu suala hili utapatiwa ufumbuzi kupitia mchakato wa mabadiliko ya Katiba yanayotarajiwa kufanyika kabla ya kupatikana kwa Katiba mpya ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

**MHE. CHRISTOWAJA G. MTINDA**: Mheshimiwa Naibu Spika, nina maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza, kwa kuwa swali langu lilikuwa linahusu ni kwa namna gani Wabunge ambao ni Wakuu wa Mikoa na Wilaya wanatimiza majukumu yao ya Kibunge na jibu lililotolewa ni kwamba wanatimiza kutokana na Ibara ya 63(3)(a) – (e).

Swali langu; kwa kuwa Ibara hiyo inasema kwamba Wabunge kazi yao kubwa ni kuishauri na kuisimamia Serikali na iliwahi kutokea hapa Bungeni Wakuu wa Wilaya kadhaa waliwahi kuuliza maswali yao Bungeni na aliyekuwa kwenye kiti wakati huo aliwaambia wao ni sehemu ya Serikali kwa hiyo hawawezi kuuliza Serikali kwa sababu wao ni sehemu ya Serikali.

Je, katika Ibara hiyo ni kwa namna gani Wabunge hawa wametimiza majukumu yao ya kuishauri na kuisimamia Serikali?

Swali la pili; kwa kuwa jibu limesema kwamba huu mwingiliano wa hii mihimili ya dola uko katika mchakato unaendelea wa Katiba Mpya. Sasa hivi bado tunaendelea kutumia Katiba ambayo ipo na Wabunge hao ambao wamo humu ndani bado wanaendelea na majukumu yao ya kuwa Wakuu wa Wilaya na Wakuu wa Mikoa na wote ni Wabunge wa Viti maalum. Nia ya kuanzishwa Viti Maalum ni kumfanya Mbunge wa Viti Maalum aweze kupata uzoefu ili baadaye agombee Jimbo. Kwa namna hiyo Wabunge hawa wa viti maalum ambao wanapangwa katika Wilaya au Mikoa ambao hawajatoka kupitia Wabunge wa Viti Maalum; ni kwa namna gani watapata uzoefu katika maeneo yao ili wasimame kugombea Majimbo kama ambavyo tunatakiwa sasa hivi? Ahsante sana. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Christowaja ukagombee Jimbo la nani? Mheshimiwa Waziri wa Nchi majibu. (*Kicheko*)

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, URATIBU NA BUNGE:** Atagombea Jimbo la Singida Kusini sijui Kaskazini.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kumkumbusha Mheshimiwa Mtinda kwamba Wakuu wa Wilaya na Wakuu wa Mikoa kama nilivyosema sio Maafisa Waandamizi wa Serikali, hawa ni *political leaders* na ndiyo maana Sheria inayotumika kwao ndiyo inatumika kwetu hata kwenye mafao.

Kwa hiyo, unatakiwa ujue tu kwamba hawa ni *political leaders* hivyo bado nasisitiza kwamba hakuna lolote ambalo limekiukwa katika Sheria hii. Lakini pia kufanya kazi kule bado wanatimizia majukumu yao ya kusimamia Serikali wakiwa hapa na bado wanasaidia Serikali katika kutekeleza yale maamuzi ambayo yamepitishwa na Bunge. Kwa hiyo, hakuna mgongano wowote.

Ni kama mimi hapa, mimi ni Mbunge lakini pia ni Waziri natumia Sheria ileile. Nafanya kazi ya Serikali lakini bado natekeleza majukumu yangu ya Kibunge na wananchi wangu hawalalamiki na wanapata raha kama vile unavyowakilisha wewe. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mtinda nataka nikuhakikishie kwamba hakuna mgongano wowote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka ieleweke kwamba nia ya Serikali pia ni kuwafanya hawa Wabunge hawa wa Viti Maalum vijana walioteuliwa kuwapa uzoefu namna ya kuendesha Serikali, namna ya kutawala. Si suala la kusimamia Serikali lakini pia namna ya kuongoza. Ni namna nzuri ambayo tumejiwekea kuandaa viongozi wa baadaye na ndiyo maana utakuta kada ya Wabunge walioteuliwa humu ndani ni vijana ambao ndiyo wanarithishwa madaraka ya baadaye.

Kwa hiyo, nataka nikwambie kwamba hakuna hitilafu yoyote lakini pia hakuna anayewakataza kuuliza maswali hapa. Hakuna, tumewasikia wakichangia hapa *unless* mimi peke yangu ndiyo nimesikia.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wakuu wa Wilaya wengi wamechangia hapa, wameishauri na wameisimamia Serikali kwa kauli na maneno yao na kama mnabisha hilo nitakwenda kuchukua Hansard ili niwaonyeshe. Hakuna hata mtu mmoja wala Kanuni zetu hazimzuii Mkuu wa Wilaya au Mkuu wa Mkoa kusema ndani ya Bunge hili hapana.

Sisi Mawaziri ndiyo tunaweza tukachangia hoja ambayo imewasilishwa na Waziri mwingine au hoja ambazo zimeletwa na Wizara husika. Lakini Wakuu wa Mikao na Wilaya wanaweza kuchangia hoja yoyote ya Serikali wakiwa ndani ya Bunge hili. *(Makofi)*

Na. 458

**CDA Kuwezesha Makao Makuu ya Serikali Kuhamia Dodoma**

**MHE. FELISTER A. BURA** aliuliza:-

Serikali iliunda Mamlaka ya Ustawishaji Makao Makuu *(CDA)* kwa lengo la kustawisha Mji wa Dodoma na kuiwezesha Serikali kuhamishia Makao Makuu yake Dodoma.

(a) Je, ni kwa kiasi gani Mamlaka ya Ustawishaji Makao Makuu *(CDA)* imefanikiwa kuiwezesha Serikali kuhamia Dodoma?

*(b)* Kwa kuwa Wananchi wa Dodoma wanahitaji ardhi kwa ajili ya kujenga na kuendeleza Mji wa Dodoma na *CDA* haijagawa viwanja kwa wananchi tangu mwaka 2004 na wananchi wa Dodoma wanahitaji ardhi kwa ajili ya kujenga na kuendeleza Mji.

Je, Serikali inawaambia nini wananchi wa Dodoma?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, URATIBU NA BUNGE** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Felister Aloyce Bura, Mbunge wa Viti Maalum, Mkoa wa Dodoma, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, wakati nilipokuwa najibu swali namba 778 la Mheshimiwa David Mchiwa Malole, Mbunge wa Dodoma Mjini, swali Namba 147 la Mheshimiwa Anne Kilango Malecela, Mbunge wa Same, Mashariki, hapa Bungeni yaliyohusu Serikali kuhamia Dodoma nililieza Bunge lako Tukufu kuwa:-

Serikali itahamia Dodoma baada ya kufikia hatua nzuri ya ujenzi wa miundombonu na huduma mbalimbali zinazohitajika kwa ajili ya kuweka watu wa ziada Dodoma na kuendesha shughuli za Serikali.

Ili kuiwezesha Serikali kuhamia Dodoma na imekamilisha uandaaji wa Mipango Kabambe ya Mji wa Dodoma, Upimaji na ugawaji wa viwanja 63,954 vya makazi na biashara, ujenzi wa barabara na mirefeji ya maji ya mvua, utandazaji wa mabomba ya mfumo wa majisafi na majitaka katika maeneo yaliyopimwa, ujenzi wa nyumba za Serikali 300 na nyumba nyingine 480 zinazomilikiwa na *CDA* na kupangishwa kwa watu mbalimbali.

Aidha *CDA* imetoa viwanja kwa ajili ya kujenga ofisi kwa baadhi ya Wizara na Taasisi; kutenga eneo la kujenga kiwanja cha ndege cha kimataifa na kutenga na kupima eneo la kituo cha kisasa cha mabasi. Vilevile, Serikali imepandisha hadhi Hospitali ya Mkoa wa Dodoma kuwa Hospitali ya Rufaa na imeanza mchakato wa maandalizi ya Sheria ya Mji Mkuu wa Dodoma. Lakini pia hivi sasa inajenga Kituo Kikubwa cha Upimaji wa Magonjwa ya Binadamu Tanzania pale *UDOM,* Dodoma.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, siyo kweli kuwa *CDA* haijagawa viwanja kwa wananchi tangu mwaka 2004. Kumbukumbu zinaonyesha kuwa kati ya mwaka 2004 hadi 2008 jumla ya viwanja 10,289 vilipimwa na kumilikishwa kwa wananchi wa viwanja 9,479 vilifanyiwa maboresho.

Aidha kuanzia mwaka 2008 hadi sasa Mmalaka imekamilisha upimaji wa viwanja zaidi ya 9,000 katika maeneo mbalimbali. Baadhi ya viwanja hivi vimeshaanza kugawiwa kwa wananchi ambao wanatakiwa kulipia gharama za usanifu, upimaji, fidia na ufunguaji wa barabara katika maeneo hayo. *(Makofi)*

**MHE. FELISTER A. BURA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Pamoja na majibu hayo ya Serikali. Kwa kuwa katika Mpango wa Maendeleo wa Mwaka 2025, Mpango wa Serikali wa kuhamia Dodoma haukuonyeshwa. Pamoja na hayo suala la kuhamia Dodoma haupo kwenye Mpango huo wa Serikali.

Je, Serikali inawaambia nini wananchi wa Dodoma?

Swali la pili, kwa kuwa tunashuhuduia majengo makubwa ya Wizara mbalimbali za Serikali zikiendelea kujengwa katika Jiji la Dar es Salaam na kwa kuwa *CDA* ambayo ilipewa jukumu la kuendeleza Mji wa Dodoma inapewa shilingi milioni 500/- kama fedha za maendeleo na hata kwa mwaka wa fedha uliopita fedha za maendeleo hazikufika kama ilivyopangwa katika Bajeti ya Serikali.

Je, Serikali ina nia kweli ya kuhamia Dodoma?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, URATIBU NA BUNGE**: Mheshimiwa Naibu Spika, anasema suala la kuhamia Dodoma halipo katika mpango wa maendeleo wa *Vision 2025.* Lakini nataka kumhakikishia mpango wa kuhamia Dodoma uko kwenye nyaraka muhimu zaidi kuliko hii kwa sababu uko katika sera ya Chama cha Mapinduzi ambayo ndiyo inaongoza Dira ya Maendeleo ya 2025.

Kwa hiyo nataka Mheshimiwa Felister Bura ajue kwamba kwa madaraka, kwa uongozi na uendeshaji wa nchi sera ya Chama cha Mapinduzi ni kubwa na ni nyaraka kubwa zaidi kuliko Dira 2025. Kwa sababu Dira 2025 inatokana na sera na miongozo ya CCM. Kwa hiyo, hilo ni jambo kubwa na limeainishwa katika sera ya Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili kwamba *CDA* haipati fedha za maendeleo na imepata milioni 500/-, hapana. *CDA* imepata fedha za maendeleo nyingi zaidi kuliko Halmashauri nyingi. Serikali imetoa fedha kupitia mkopo uliochukuliwa na Serikali *World Bank* zaidi ya shilingi bilioni 32/- ambazo zinatekeleza mradi mkubwa wa miundombinu katika Dodoma na nyie wote Waheshimiwa Wabunge ni mashahidi.

Barabara nyingi sana zinajengwa, mifereji ya majitaka inajengwa hapa mjini zote hizi ni fedha za maendeleo. Fedha za maendeleo kwa tafsiri sio fedha zile tu za madafu zinazokusanywa kwa kodi za Watanzania. Fedha za maendeleo ni zote zinazotengwa na Serikali hata zile ambazo fedha zinazotoka nje ya nchi. Ndiyo maana Dodoma imependelewa kupewa fedha hizi nyingi zaidi kuliko Halmashauri zote zinazotekeleza mradi huu. Dodoma imepewa mara mbili ya kiwango ambacho Halmashauri nyingine zimepewa. Kwa hiyo fedha za maendeleo zipo na kazi kubwa inaendelea na hii ni awamu ya kwanza. Tunaendelea na uboreshaji wa miundombinu Dodoma mpaka tutakapomaliza miundombinu yote ambayo inakusudiwa kwa Makao Makuu, Dodoma.

**MHE. ENG. MUHAMMED HABIB JUMA MNYAA**: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa fursa ya kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa dhamira ya Serikali kuhamia Dodoma ni ya muda mrefu na kuna nchi zilihamisha Makao Makuu yao na zikaja Tanzania kufuata au kuiga na kutizama mipango ya Tanzania kama vile Lilongwe na Abuja miaka mingi iliyopita.

Wao wamejenga Makao Makuu yao na wamehamia miji hiyo na kwa kuwa jibu hili la kujenga miundombinu,

kiwanja cha ndege, nyumba 350 ni majibu hayo hayo yanayotolewa na Serikali. Kwa kuwa hivi sasa pia kuna mpango wa kuendeleza Mji wa Kigamboni ambao tunaona nguvu kubwa ya Serikali inaelekezwa huko kuliko Dodoma.

Je, ni mipango gani hiyo unayosema ni zaidi ya *vision 2025* ni sera ya CCM kwamba jambo moja halijakamilika kwa muda wa zaidi ya miaka 25 sasa kunaelekezwa nguvu kwenye mji mwingine? Tupe sababu na hiyo mipango kwanini haijafanyika?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, URATIBU NA BUNGE**: Mheshimiwa Spika, ni kweli nchi nyingi kama alivyosema Nigeria wamejifunza. Lakini sio hizo tu Tanzania ni mwalimu wa mambo mengi sana. Tanzania kutokana na busara ya viongozi wetu na sera nzuri za vyama vyetu *TANU, ASP* na CCM hatuwezi kuacha hilo, wala sio la kuhamia Dodoma tu, hata ukombozi. *Base* ya ukombozi ni Tanzania katika nchi zote za Kusini mwa Afrika. Kwa hiyo, suala la kujifunza Tanzania usilione tu hilo la kujenga Mji Mkuu Dodoma, mambo mengi sisi tumewafundisha na tunawakaribisha wataendelea kujifunza.

Lakini pia sisi tunajenga Mji wa Dodoma kwa utaratibu wetu. Haiwezekani Abuja wamejenga kwa miaka miwili kama unavyosema kwa muda mfupi na sisi tukaiga hapana. Sisi tunayo *Master Plan* yetu na tunakwenda kulingana na *Master Plan* tuliyoipanga na utaratibu wetu. Hii ni Serikali huru na lazima iendeshwe kwa mipango yake ya ndani. Hatuwezi kuiga Abuja walivyofanya.

Lakini iko tofauti kubwa kati ya Mji wa Kigamboni na Dodoma. Mji wa Kigamboni ule umewekwa maalum kwa ajili ya wawekezaji binafsi, sio mji wa Serikali. Dodoma ni Makao Makuu ya nchi. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mnyaa umetoa mifano miwili tofauti. Unguja ni Mji vilevile Dodoma tunajenga Makao Makuu lakini huwezi kusema Pemba ni sawa na Dodoma hapana, ingawa Pemba ni Mji. Dodoma ni Mji lakini ni Makao Makuu. Unaona hiyo inayoongezeka. Makao Makuu. Kwa hiyo, hiyo ndiyo tofauti kati ya Kigamboni na Dodoma.

**MHE. HEZEKIA H. N. CHIBULUNJE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi niulize swali dogo la nyongeza, wananchi wa Dodoma wangependa wapate nia thabiti kabisa ya Serikali kuhamia Dodoma kwa sababu tumeshuhudia hivi karibuni baadhi ya Taasisi za Serikali zilikuwa ziko hapa Dodoma zimepewa ruhusa kuhamia Dar es salaam. Lakini vilevile ninazo taarifa kuwa kuna tetesi za Idara za Serikali zilizokuwa hapa nazo zinajipanga kuhamia Dar es salaam. Nia thabiti ya Serikali kuhamia Dodoma iko vipi katika msimamo huo?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Nchi nia thabiti majibu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, URATIBU NA BUNGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nijibu swali la nyongeza la Mjomba wangu Mheshimiwa Chibulunje Mbunge wa Chilonwa kama ifuatavyo pamoja na wewe Mheshimiwa Naibu Spika, Mjomba wangu ninakujibu.

Nia ya kuhamia Dodoma, nia ya Serikali ya kuufanya Mji wa Dodoma kuwa Mji Mkuu ipo pale pale. Kwa hiyo kama hii inatosha basi ichukuliwe kama ndiyo kauli thabiti ya Serikali, kuwa nia ya Serikali ya kuwa na Makao Makuu Dodoma iko pale pale na Serikali itaendeleza mipango yote inakusudia na inayotaka kuitekeleza ili kuifanya Dodoma iwe Makao Makuu ya nchi yetu.

Hizo fununu anazosema kuwa Wizara za Serikali zinahamia Dar es Salaam, hapana tunayo Wizara ya TAMISEMI, Ofisi ya Waziri Mkuu ninazungumza kwa niaba ya Waziri Mkuu yuko hapa, Waziri wake na Wizara hii iko Dodoma.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali haijatangaza mpango wowote wa kuhamisha Makao Makuu ya Ofisi hii kubwa kabisa ya TAMISEMI hapa Dodoma hakuna. Kwa hiyo, Mheshimiwa Chibulunje na Waheshimiwa wengine wananchi wa Dodoma hizo habari za uvumi ninafikiri siyo za uhakika uhakika ni huu ninaousema mimi hapa kwa sababu mimi niko Ofisi ya Waziri Mkuu na TAMISEMI iko Waziri Mkuu.

Kwa hiyo, hizi ni habari za uhakika kuwa TAMISEMI iko Dodoma.

Mheshimiwa Naibu Spika, *LAPF* ni Shirika lina wenyewe, wafanyakazi wamewekeza katika Shirika la *LAPF* Mifuko yote Makao Makuu yake wamefanya ni Dar es salaam. Kwa hiyo, ili kuleta ushindani na kutoa huduma bora zaidi kwa wanachama wake ambao ndiyo wenye mfuko ni kweli kuwa sasa Makao Makuu yanke sehemu kubwa siyo kwamba wanavunja hii inagawa mkiangalia pale Dodoma bado wamewekeza Kitega Uchumi kikubwa sana na wameendelea kuwekeza na *UDOM* lakini kwa kiasi kikubwa watahamia Dar es salaam, kwa sababu mifuko mingine yote iko Dar es salaam na sehemu kubwa ya Wanachama wake ni rahisi zaidi kupafikia Dar es salaam na wengi zaidi wako Dar es salaam na *LAPF* kwa kiwango fulani na yenyewe inafanya biashara.

Ili mtandao wake wa biashara uweze kukamilika imeonekana ni vizuri wakiwa Dar es salaam ili waweze kutekeleza mipango yao vizuri, lakini hiyo haimaanishi na wala haina mahusiano ya kuondoa Makao Makuu Dodoma.

**NAIBU SPIKA:** Tunakushukuru sana Waziri na pole sana kwa maswali hayo. Waheshimiwa Wabunge mmekaa hapa miezi karibia miezi miwili, mitatu kama kweli mmepata nafasi ya kutembelea Mji wa Dodoma mtaona mabadiliko ni makubwa sana ya maandalizi ya ujenzi wa Dodoma. Tunaipongeza sana Serikali kwa hilo, ni Swali la Mheshimiwa Jeremiah Meshack Opulukwa.

Na. 459

**Matatizo Makubwa ya Walimu Meatu**

**MHE. MESHACK J.OPULUKWA** aliuliza:-

Liko tatizo kubwa la walimu wa Meatu kucheleweshwa kupandishwa cheo na pia pale wanapopandishwa daraja hawalipwi stahili zao:-

Je, ni lini Serikali itashughulikia na kuyaondoa kabisa haya matatizo yanayowakabili walimu wa Meatu?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI (ELIMU):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Meshack Jeremiah Opulukwa, Mbunge wa Meatu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imedhamiria kuondoa tatizo la walimu kuchelewa kupandishwa madaraja na kulipwa stahili kama ifuatavyo:-

- Kuimarisha na kuboresha mfumo wa taarifa za Utumishi na Mishahara Serikalini *LAWSON* kwa kuwekea taratibu za kiutumishi za kushughulikia malimbikizo ya mishahara, kuhamisha, ukomo wa utumishi na marekebisho ya taarifa za mtumishi.

- Katika mwaka wa fedha 2013/2014, Serikali itaboresha idara ya Utumishi wa walimu *(TSD)*kifedha na rasilimali watu ili iweze kumudu majukumu ikiwemo upandishwaji madaraja walimu.

- Aidha Serikali imeunda Kamati ya kuchambua na kutoa mwongozo kwa ajili ya kushughulikia changamoto ya upandishwa madaraja walimu. Mwezi Januari, 2013, mapendekezo ya Kamati yaliwasilishwa katika Baraza la majadiliano ya pamoja katika ya sekta Elimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imetoa maelekezo kwa Wakurugenzi wa Halmashauri wote nchini kutosababisha madeni na kuhakikisha kuwa wanatenga fedha za kuwapandisha madaraja watumishi wakiwamo walimu na kuhakikisha marekebisho ya mishahara yanalipwa kwa wakati. Mwaka wa fedha 2013/2014, Serikali imetenga nafasi za kuwapandisha vyeo walimu 39,602 walio katika Mamlaka ya Serikali za Mitaa na shilingi milioni 64 zimetengwa kwa ajili ya kuwapandisha madaraja walimu 330 wa Halmashauri ya Wilaya ya Meatu.

Serikali itaendelea kuwajengea uwezo watendaji ili waweze kutumia mfumo wa *HCMIS* kikamilifu na kutatua changamoto zilizopo. *(Makofi)*

**MHE. MESHACK J. OPULUKWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa kuna walimu zaidi ya 100 kwenye Halmashauri ya Meatu ambao walipandishwa daraja mwaka jana mwezi wa nne, lakini baadaye mwezi huohuo wakati walikuwa wamepewa barua za kupandishwa madaraja walinyang'anynywa zile barua kuwa zilikosewa na kurudishwa *TSD,* sasa ni lini walimu hawa ambao wameshapanda daraja toka mwaka jana mwezi wa nne watapata stahili zao kama ambavyo barua zilivyokuwa zikielekeza kabla ya kunyang'anywa?

Swali la pili. Kuna walimu ambao waliomba likizo wakaruhusiwa kwenda likizo kwa mujibu na taratibu za uombaji wa likizo, lakini kati ya walioomba likizo ni baadhi yao tu ndio ambao walilipwa fedha ya kwenda likizo.

Je, ninapenda kuuliza ni taratibu zipi zilizotumika kuwabagua walimu hawa baadhi wakalipwa lakini wale wengine hawakuweza kulipwa fedha zao za likizo? Ahsante sana.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI (ELIMU):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ninaomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Meshack Opulukwa, Mbunge wa Meatu, kama ifuatavyo:-

Upo ukweli kuwa Tume ya Utumishi Ofisi ya Rais ilitoa maelekezo ya mfumo wa upandishaji wa madaraja ambayo mwezi Januari walisitisha kufanya hivyo kwa Watumishi wote nchini wakiwemo walimu na kibali hicho kimetolewa tena mwezi Aprili ili kuendelea na mchakato wa upandishaji wa madaraja baada ya kuondoa kasoro amabzo zilikuwa zimejitokeza na kwa hiyo walimu wale ambao walinyang'anywa barua zao sasa watarudishiwa na Halmashauri kupitia *TSD* pale Meatu ili mchakato ule

uendelee pamoja na uratibu wa fedha za kuwalipa walimu hawa kwenye malimbikizo yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini fedha hizi za malimbikizo mara nyingi zinalipwa na Hazina. Kwa hiyo, Halmashauri zote nchini kupitia *TSD* wanachofanya sasa ni kuratibu na kuorodhesha walimu wote ambao wamepandishwa na kubadilisha ngazi za mishahara ili rekodi zile ziende Utumishi, Utumishi watoe kibali Hazina na Hazina ianze kulipa na ulipaji wake unapitia katika *account* za walimu wenyewe moja kwa moja. Kwa hivyo, utaratibu utaendelea kupitia maelekezo haya.

Lakini swali la pili la likizo ni kweli kuwa nchi nzima tunao walimu katika kila Halmashauri wanapaswa kwenda likizo ikiwa ni haki yao ya msingi na kila Mtumishi anatakiwa kwenda likizo mara moja ile ambayo anatakiwa kulipwa fedha zake.

Kwa hiyo, inawezekana pia kuwa hela ambazo TAMISEMI tunazituma katika Halmashauri hazitoshi au hazikidhi mahitaji ya walimu wote wa Halmashauri na kwa hiyo Maafisa Elimu ambacho tumewashauri ni kuandaa orodha ya walimu wanaopaswa kwenda likizo ikiwezekana miezi kabla ya wale ambao watalipwa kulingana na fedha ambazo sisi tumepeleka ili waweze kulipwa na tumewasihi Maafisa Elimu kuimarisha mawasiliano kati yao na walimu wetu ili kuondoa tofauti ambazo zinaendelea kuwafanya walimu kuwa na uhakika wa lipi baada ya mawasiliano hayo ili kuondoa kasoro hizo za kutokuwa na taarifa ambazo Mheshimiwa Mbunge ulikuwa unahitaji.

Kwa taarifa hii kupitia Bajeti zetu za mwaka huu wa 2012/2013 tumeongeza viwango hivi vya fedha ambavyo tunatuma kwenye Halmashauri kwa ajili ya kulipa likizo ili zisaidie kuongeza idadi ya walimu wanaokwenda likizo kama haki yao ya msingi ili walimu hawa waweze kulipwa fedha zao zote. Kwa hiyo, huo ndiyo utaratibu tunaotumia katika Halmashauri zetu.

**NAIBU SPIKA:** Nimekuona Mheshimiwa Dkt. Mary Mwanjelwa, swali moja la nyongeza.

**MHE. DKT. MARY M. MWANJELWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru sana kwa kuniona kwa kuwa tatizo la walimu wa Meatu linafanana sana na Walimu wa Jiji la Mbeya licha ya kwamba walimu wa Jiji la Mbeya, wamecheleweshwa sana kupandishwa madaraja, lakini pia wanashushwa madaraja na walimu hawa wa Jiji la Mbeya unakuta wamejiendeleza mpaka Vyuo Vikuu, lakini ajabu ni kwamba wanaambiwa kwamba kupandishwa kwao madaraja kulikosewa hawajalipwa stahili zao.

Kwa hiyo, nilikuwa ninataka Mheshimiwa Waziri atueleze sintofahamu hii ya walimu wa Jiji la Mbeya ni nini tatizo na lini watapewa haki zao?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI (ELIMU):** Mheshimiwa Naibu Spika, jambo hili kama nilivyoeleza kwenye jibu la nyongeza la Mheshimiwa Opulukwa linaikabili karibu kila Halmashauri nchini. Tatizo la Manispaa ya Mbeya ninalifahamu, hatuna Katibu wa *TSD* Mbeya, suala hili la Katibu wa *TSD* ni la Ofisi ya Rais Utumishi ambalo linapaswa kuwapeleka Makatibu wa *TSD* na Mkoa mzima wa Mbeya. Tuna Makatibu wasiozidi watano katika Halmashauri zote saba. Kwa hiyo, bado tuna upungufu wa Makatibu *TSD* ambao watafanya kazi ya kuwapandisha walimu hawa. Usitishaji wa kutopandisha madaraja kwa Watumishi wote uliofanywa na Utumishi ulitoa nafasi ya kufanya uratibu kwenye maeneo haya lakini kwa Manispaa ya Mbeya tumetoa maelekezo ya kuhamisha Katibu *TSD* kutoka Rungwe mmoja aende Manispaa ili kuokoa tataizo hili ambalo linawakabili sana walimu wa Manispaa ya Mbeya.

Hii sasa akishakuwa pale ataweza kutatua matatizo ya msingi ingawa atakuwa na kazi kubwa ya kuweza kupitia ucheleweshaji ambao umejitokeza katika Manispaa ile ili kuwafanya walimu hawa. Hii itakuwa ni pamoja na malipo yao kama ambavyo nimeeleza kwenye jibu la nyongeza la Mheshimiwa Opulukwa.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, ninawaona lakini muda hauko upande wetu. Swali la Mheshimiwa Dkt. Augustine Lyatonga Mrema, kwa niaba yake Mheshimiwa James Mbatia.

Na. 460

**Kesi Inayozuia Mji wa Himo Usipimwe Viwanja**

**MHE. JAMES F. MBATIA (K.n.y. MHE. DKT. AUGUSTINE LYATONGA MREMA)** aliuliza:-

Inasemekana kuwa kesi bandia tangu 2002-2013 inayozuia Mji wa Himo usipimwe viwanja na kujengwa.

(a) Je, inakuwaje kesi inakaa Mahakamani kwa miaka zaidi ya kumi (10) bila kumalizika?

(b) Je, Serikali inakusudia kumaliza vipi mgogoro wa viwanja Himo?

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu na kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Augustine Lyatonga Mrema, Mbunge wa Jimbo la Vunjo, naomba kutoa maelezo ya utangulizi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kuwa ipo kesi Na. 1/2003 iliyofunguliwa na Ndugu Augustino Temu na Paul Lyimo kwa niaba ya wananchi wengine 345 dhidi ya Halmashauri ya Wilaya ya Moshi Vijijini, wakipinga upimaji wa viwanja katika eneo la Mji wa Himo kwa madai kwamba eneo linalotakiwa kupimwa ni eneo la asili hivyo hawakubaliani na upimaji huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo mafupi sasa ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Augustine Lyatonga Mrema, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a)Mheshimiwa Naibu Spika, kesi hii imechukua muda mrefu kwa sababu kumekuwa na maombi mengi kutoka kwa walalamikaji wa kesi hii. Mfano maombi ya hayo ni maombi Na.1/2008, yaliyowasilishwa Mahakamani na walalamikaji kuitaka Halmashauri kuthibitisha kama upimaji wa viwanja uliokwishafanyika ulifuata taratibu za upimaji na maombi Na. 14/2012 ambayo walalamikaji wameomba Mahakama kuzuia upimaji wa viwanja katika eneo hili mpaka kesi itakapomalizika.

Ninapenda kuliarifu Bunge lako kwamba maombi haya mawili tayari yamekwisha sikilizwa na hivi sasa tunachokisubiri ni Mheshimiwa Jaji aliyekuwa akisikiliza kesi hii aweze kwenda kuimalizia kusikiliza na tunaamini kuanzia mwezi julai mpaka August mwaka huu 2013 kesi hii itakuwa imemalizika.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa kesi hii bado iko Mahakamani, Serikali haiwezi kuingilia maamuzi ya Mahakama na kwamba inasubiri maamuzi yatolewe ndipo shughuli za upimaji wa viwanja ziweze kuendelea katika eneo lenye mgogoro. Hivyo, kumalizika kwa mgogoro huu kutategemea maamuzi yatakayotolewa na Mahakama kufuatia kesi inayoendelea. *(Makofi)*

**MHE. JAMES F. MBATIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa mradi huu wa kupima Mji wa Himo na Miji mingine unahitaji sana *Future Master Plan* ya Miji yetu yote ikiwemo Dodoma, Dar es salaam na kwingineko Serikali haioni kwamba kabla ya kuanzisha mradi wowote ule kuna *idea concept physibility study for project realization na Project* Management na inategemea *sana time, cost and quality* sasa kesi hii imekuwa Mahakamani kwa zaidi ya miaka kumi na moja sasa.

Ni nini *communication strategy* ya Serikali kwa sababu ya *integration* ya *time kwa* wakati huu ili kuweza kuondoa muda umekuwa mrefu ili *project* hii ya Himo na *Future Plans* za Miji mingine yote tuwe na maabara ya kufikiri badala ya

kuingiza Taifa kwenye migogoro kama hii inayoendelea Himo sasa hivi kwa ajili ya maendeleo endelevu ya Taifa letu?

Haki inayocheleweshwa ni haki inayonyimwa, Mheshimiwa Naibu Waziri kwa nini kusiwepo na meza ya mazungumzo nje ya Mahakama. *You better have a bad settlement outside the court rather than Judgment in the Court* ili kuweza kumaliza mgogoro huu tuweze kuokoa muda na Miji yetu iweze kupanuka nchi nzima?

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA**: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ninaomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa James Mbatia, Mbunge wa kuteuliwa, kama ifuatavyo:-

Swali la kwanza, Serikali ina *communication strategy* gani ya kuhakikisha kuwa kesi hii inamalizika ninadhani katika jibu langu la msingi nilishaeleza kuwa tunatarajia ndani ya mwezi Julai mpaka mwezi August kesi hii itakuwa imekwisha malizika, na ninapenda tu kulieleza Bunge lako Tukufu kuwa kesi hii imeshikiliwa na Majaji watatu Jaji Mziray aliyeko sasa hivi ni Jaji wa tatu na suala hili limekuwa likichelewa kutokana na walalamikaji wenyewe wa kesi hii na kama ambavyo Mheshimiwa Mrema mwenyewe ameuliza kesi hii imekuwa ikionekana ni kesi ya bandia kwa sababu hata hao walalamikaji wengine 345 hawajawahi kuthibitisha kama kweli ni walalamikaji katika kesi hii.

Lakini pia suala kubwa katika kesi hii imekuwa ni mgogoro wa namna bora ya kufikia kiwango cha fidia wamekuwa wakikaa na kama ambavyo mwenyewe umekwishakueleza katika swali lako namba mbili, kuwa ni kwa nini badala kutumia usuluhishaji wa Mahakama kwa nini hatutumii mbinu zingine kusuluhisha mgogoro huu kama ambavyo nimeshaeleza katika maombi ya pamoja ya mwaka 2008 na maombi namba 14 ya mwaka 2012.

Mheshimiwa Jaji Mziray alielekeza kesi hii iende katika hatua ya usuluhishi na imekuwa ikifanyika lakini meza ya

mazungumzo wao wenyewe walalamikaji wamekuwa wakishindwa kufikia muafaka na ndiyo maana imeondoka katika hatua hiyo tumeshamaliza maombi yale sasa hivi mwezi wa saba na mwezi wa nane Mheshimiwa Jaji Mziray akienda ni kuimaliza kabisa. Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Swali fupi sana la nyongeza Mheshimiwa Joseph Selasini, nilikuona.

**MHE. JOSEPH R. SELASIN:** Mheshimiwa Naibu Spika**,** kesi bandia zinazofanana na kesi hii zipo nyingi katika Mahakama zetu hapa nchini. Je, ni lini Serikali itafanya utafiti wa kesi kama hizi na kutumia njia za usuluhishi ili ziondoke Mahakamani kwa ajili ya kujenga dhana ya kuwapatia wananchi haki ambayo wanaitafuta kwa muda mrefu?

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Selasini ametaka kujua ni lini Serikali itafanya utafiti wa kufahamu kesi zilizorundikana katika Mahakama zetu ambazo zinaonekana labda ni za bandia kama hii ya Mji wa Himo.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba Serikali kupitia Mahakama ipo katika mpango wa kufanya uchambuzi kesi zote zilizoko Mahakamani, kuzipitia kwa kina, kuangalia zimewasilishwa mahakamani hapo mwaka gani, lakini si hilo tu, tuna mpango kuanzia mwezi huu julai mwaka 2013 kuanza na Mji wa Arusha, Mji wa Mwanza pamoja na Jiji la Dar es Salaam, tunaanzisha Kamati inayoitwa *Bench Bar Judiciary Committee.*

Katika Kamati hii tutakaa Uongozi wa Mahakama pamoja na Uongozi wa Mawakili ili kupitia kesi zote na kuwapa taarifa kwa wale Mawakili ambao wanajulikana kwa kuweka pingamizi Mahakamani watataarifiwa mbele ya Mawakili wenzao ili waone kama kweli ni sahihi kesi hizi kupigwa danadana kwa muda mrefu kama ambavyo umeelezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini si hiyo tu, ukiangalia katika Mahakama Kuu kitengo cha ardhi, jana tarehe 24 tumeshaanza vikao vya Mahakama katika Mkoa wa Mtwara, Tanga na katika Mkoa wa Mwanza. Tunaandaa programu pia nchi nzima na tutaweka kalenda hiyo wazi kabisa ili tuweze kumaliza kesi zote zenye mlundikano. Katika Mahakama ya ardhi tayari sasa hivi tumeanza na kesi zote zza mwaka 2009 na tutakuja za mwaka 2010, 2011 mpaka hivi sasa. Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Tuendelee na ofisi ya Makamu wa Rais Mazingira, swali linaulizwa na Mheshimiwa Mhandisi Athumani Mfutakamba.

Na. 461

**Uhifadhi wa Mazingira**

**MHE. ENG. ATHUMANI R. MFUTAKAMBA** aliuliza:-

Baada ya Mkutano wa kwanza wa uhifadhi wa mazingira duniani kumalizika mwaka 1992 huko *Rio De Janerio,* sasa ni miaka ishirini na moja (21) imepita:-

(a) Je, Serikali imeweka utaratibu gani wa kulinda athari za mabadiliko ya tabianchi na kupeleka elimu vijijini ambako kunatokea mafuriko na ukame?

(b) Je, baada ya mazungumzo ya Doha na Cancum, Tanzania imejipangaje kuzuia hasara na upotevu wa mali unaotokana na Nchi za Ulaya, Marekani, China na India ambazo zinachangia kwa kiwango kikubwa kuingiza hewa ya ukaa *(CO2)* kupitia viwanda vyao duniani?

(c) Je, Serikali itawasaidiaje wananchi wa Igalula na maeneo mengine nchini yaliyokumbwa na ukame uliosababisha mazao na mifugo kufa miaka mitatu mfululizo kutoka na athari ya tabianchi?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MAZINGIRA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Eng. Athuman Rashid Mfutakamba, Mbunge wa Igalula, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Serikali imeweka utaratibu wa kuendesha vipindi vya redio na runinga na maadhimisho mbalimbali ya mazingira kuhusu athari za mabadiliko ya tabianchi na namna ya kukabiliana nayo.

Aidha Serikali ina washirikisha Watendaji katika ngazi za Halmashauri na wanavijiji katika utekelezaji wa miradi inayohusu mabadiliko ya tabia nchi. Kwa mfano tangu mwaka 2011/2012 Serikali inatekeleza miradi ya vijiji vya mfano *eco-villages* katika vijiji vya Chololo Mkoani Dodoma, Luguru Morogoro na Zanzibar chini ya ufadhili wa Jumuiya ya Ulaya.

Vilevile utekelezaji wa mradi wa kuhimili mabadiliko ya tabianchi unaofanyika ili kuwezesha upatikanaji wa maji katika Wilaya za Igunga, Mbinga, Misenyi kwa upande wa Tanzania Bara na Chakechake kwa upande wa Zanzibar.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya mikutano ya Cancun na Doha, na *Durban - South Africa,* Tanzania imekamilisha kuandaa mkakati wa Mabadiliko ya Tabianchi ambao unatoa mwongozo wa hatua zinazotakiwa kuchukuliwa na sekta mbalimbali katika kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi.

Ili kutekeleza mkakati huo baadhi ya sekta zimeanza kuandaa mipango ya utekelezaji. Kwa mfano Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika na Wizara ya Maji zimeshaanza maandalizi ya kuandaa mipango ya aina hiyo. Aidha Serikali imeandaa mpangokazi wa kuandaa mpango wa muda wa kati na muda mrefu wa kukabili mabadiliko ya tabianchi katika sekta mbalimbali.

Vilevile Serikali inaendelea kutekeleza miradi miwili mikubwa ya kuhimili mabadiliko ya tabianchi inayofadhiliwa na mfuko wa nchi maskini duniani na mfuko wa dunia wa kuhimili mabadiliko ya tabianchi *(Adaptation Fund –AF)* katika ukanda wa Pwani.

(c) Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inawashauri wananchi wa Igalula na maeneo mengine nchini kuzingatia ushauri unaotolewa na watalaam wa Kilimo na Mifugo katika maeneo hayo kuhusu aina ya mazao yanayoweza kustawi na ufugaji wenye tija.

Aidha, wananchi na wkaulima wanashauriwa kuzingatia ushauri unaotolewa na Mamlaka ya hali ya hewa nchini kuhusu mwenendo wa hali ya hewa.

**MHE. ENG. ATHUMAN R. MFUTAKAMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa majibu mazuri ya Waziri, nina maswali mawili madogo ya nyongeza.

Swali la kwanza, biashara ya hewa ukaa katika misitu inayomilikiwa na *green resources* kule Mufindi pamoja na Muheza na Manyara wanafaidika kwa biashara hiyo, Waziri anaweza kuniambia utaratibu huo unaweza kusaidiwa kwa vijiji vya Igoweko, Mienze, Luoya na Lutende pamoja na Tura ambao wanahifadhi misitu ya vijiji kwa kutumia mpango wa *PFM (Participatory Forest Management)* ili nao waweze kufaidika kwa fedha za kutoka Ulaya na Marekani?

Swali la Pili, kwenye agenda ya 21 kulikuwa na suala mtambuka la Nishati Mbadala Vijijini.

Je, Wizara ya Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira ikishirikiana na Wizara ya Nishati na Madini wanaweza kusaidiaje wananchi wa Igalula ili wasiendelee kukata miti kwa ajili ya mkaa na kuni na kupata nishati mbadala ya sola pamoja na *biogas* kama wanavyofanya Thailand? Nashukuru sana.

**NAIBU SPIKA:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Mheshimiwa Terezya Pius Luoga Huvisa Gama (*Kicheko/Makofi*)

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MAZINGIRA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza napenda kutoa shukrani kwa kunitambua kwa majina yangu yote. Ahsante sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu biashara ya hewa ukaa ambayo inaendeshwa na kampuni ya *green resource*, ninachoweza kusema ni kwamba ni kweli *green resource* kutoka Serikali ya Norway ndiyo wamekuwa Taifa la kwanza kuendesha hii biashara, lakini biashara hii ya Kimataifa ina taratibu zake na ninapenda kuwaelimisha wananchi wote kupitia Bunge lako Tukufu kwamba Biashara hii inatakiwa mwekezaji pamoja na mwananchi wapewe gawio. Gawio ni lazima liwe nusu kwa nusu. Wanachofanya *green resource* wanatoa gawio la *ten percent* tu ambapo ni ukiukwaji mkubwa wa taratibu za kimataifa. Kwa hiyo, mpaka sasa hivi Ofisi ya Makamu wa Rais haijatoa kibali cha kuwaruhusu kuendelea na biashara hiyo mpaka watakaporekebisha taratibu hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, taratibu hizo zikikamilika, Taifa zima na sehemu zote zinazohifadhi misitu basi wataweza kufaidika na biashara hii ya hewa ukaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili linalohusu agenda ya 21 kuhusu nishati mbadala. Ni kweli kabisa kutokana na mabadiliko ya tabianchi tunahitaji kuwa na nishati mbadala na suala hili tumeshaliongelea mara nyingi sana hasa kwenye mikutano yetu ya kimataifa kwamba wakati wote nchi ambazo zinaendelea zilikuwa zinanyonya hewa ukaa bila kujua, lakini sasa hivi tumeshajua na ndiyo maana mazungumzo yanaendelea katika mikutano ya kimataifa ili nchi zinazoendelea ziweze kupata fidia ya kufanya hiyo kazi ya kunyonya hewa ukaa. Tunapopata hizo pesa, hizo pesa zitatusaidia sana kuwaelimisha wananchi na kutumia kwenye nishati mbadala.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla hatujapata hizo pesa, nitoe wito kwamba Wabunge tuendelee kuwaelimisha wananchi pamoja na kwamba tunatumia kuni na mkaa, basi tutumie majiko banifu ili tuweze kutumia kuni kidogo na mkaa mdogo. Lakini vilevile tuendelee kupanda miti kwenye mashamba yetu, tutumie kilimo mseto ili tusivune miti hiyo kwenye misitu badala yake tuvune kwenye mashamba yetu.

**NAIBU SPIKA:** Swali fupi sana la nyongeza, naomba Mwenyekiti wa Kamati ya Wabunge marafiki wa Mazingira Mheshimiwa Hilda Ngoye.

**MHE. HILDA C. NGOYE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa nafasi hii na kwa kunitambua vile vile.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa suala la mazingira ni suala la mtambuka na wote tunafahamu hivyo, na kwa kuwa huko vijijini kumeanzishwa taasisi mbalimbali zisizo na kiserikali *NGO's* ambazo zinafanyakazi nzuri sana ya kuelimisha na wameanzisha miradi midogomidogo ya kusaidia wananchi ili kudhibiti matatizo ya uharibifu wa mazingira.

Je, Serikali ina utaratibu gani wa kuzitambua hizi taasisi zisizo za kiserikali, ambazo zinafanyakazi nzuri sana kwa wananchi wetu. Serikali inawasaidiaje wananchi hawa ambao wapo kwenye vyama hivi ili waweze kuendelea kufanyakazi nzuri ya kuhifadhi mazingira?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MAZINGIRA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza niwapongeze Wabunge wote ambao wapo kwenye asasi hiyo, kwa sababu sisi Wabunge ndiyo tunaotakiwa kuwa viongozi wa kuhifadhi mazingira. Kwa hiyo, nitoe wito hata kwa Wabunge wengine waingie kwenye chama hicho cha rafiki wa mazingira ili tuweze kuonesha mfano na kuelimisha wananchi kwa ujumla. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu swali linalohusu *NGO's* pia nizipongeze *NGO's* zote ambazo zinasaidia kwa hali na mali kuhifadhi mazingira ya nchi yetu, ili maisha yetu yawe endelevu. Ninajua kabisa kuna *NGO's* nyingi ambazo ni rafiki wa mazingira, wanatoa elimu, wanafanyakazi mbalimbali, tunazitambua na kwa kutambua huko tumeanzisha mashindano ambapo Rais anatoa tuzo ya mazingira kwa wale wote ambao wamefanya vizuri na tuzo hii inafanyika kila baada ya miaka miwili. Tulitoa mwaka jana tutatoa tena mwaka kesho.

Kwa hiyo, ninaomba *NGO's* zote ziwasiliane na Mkurugenzi wa Mazingira ofisi ya Makamu wa Rais ili waweze kuingia kwenye tuzo hii. Lakini wanapowasiliana basi wapitie kwenye Halmashauri zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile kuna miradi midogomidogo ya *UNDP* ambapo Ofisi ya Rais ni mdhibiti, na kila mradi wanapata milioni hamsini. Kwa hiyo tunaomba Wabunge *NGO's* zilizoko kwenye majimbo yenu muwashauri waandike miradi hii ili waweze kupata milioni hamsini kuendeleza shughuli mbalimbali zinazofanyika na *NGO's.*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tuendelee na swali linalofuata kwa sababu ya muda, nawaona kabisa lakini muda hauko upande wangu. Swali la Wizara ya Nishati na Madini, Mheshimiwa Shaffin Ahmedali Sumar.

Na. 462

**Wilaya ya Uyui Kupatiwa Umeme**

**MHE. SHAFFIN A. SUMAR** aliuliza:-

Wilaya ya Uyui haina Hospitali ya Wilaya na pia kuna kituo kimoja cha Afya ambacho hakina huduma ya umeme.

Je, Serikali haioni umuhimu wa kupeleka umeme ambao umepita umbali wa kilomita tisa(9) tu kutoka kwenye Kituo cha Afya?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini napenda kujibu swali la Mheshimiwa Shaffin Ahmedali Sumar kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia wakala wa nishati vijijini REA inatekeleza mradi wa kuepeleka umeme Wilaya ya Uyui katika maeneo ya kituo cha Afya cha Upuge, Ndono, Ufulama, Mbutu, Mogwa, Ntubugo, Nyangabe, Muhulidede Magiri/Mayombo, Kigwa A na B, Goweko, Polisi Imalakaseko, Igalula na Inala - Tabora Mjini. Mradi huo utatekelezwa chini ya mpango kabambe wa umeme vijijini awamu ya pili.

Mheshimiwa Naibu Spika, zabuni ya kuwapata Wakandarasi wa kazi hizi ilitangazwa mwezi Desemba, 2012 na kufunguliwa mwezi Machi, 2013. Kazi za mradi huu zitahusisha:-

(i) Ujenzi wa njia ya umeme wa msongo wa KV 33 umbali wa kilomita 8;

(ii) Ujenzi wa njia ya umeme ya msongo wa Kv 0.4 umbali wa Km2;

(iii) Kufunga *transfoma* tatu zenye uwezo wa *KvA 50;* na

(iv) Kuunganisha wateja wa awali wapatao 70.

Gharama ya kazi hizi inakadiriwa kuwa shilingi milioni 451.21. Kazi hizi zinatarajiwa kuanza wakati wowote mwaka 2013.

**MHE. SHAFFIN A. SUMAR:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri, naomba niulize maswali mawili ya nyongeza.

Kwa kuwa, jirani na Kata ya Upuge kuna Kata ya Ikongolo ambapo kuna vijiji vya Kanyenye, Majengo na Ikongolo ambavyo havikutajwa kwenye jibu la msingi na badala yake kuna vijiji vingi vimetajwa ambavyo havimo Jimbo la Tabora Kaskazini.

Je, nini mpango wa Serikali wa kuvipatia umeme vijiji hivi vya Kanyenye, Majengo na Ikongolo?

Swali la pili, kwa kuwa, kuna maeneo mengi nchini ambayo yamepitiwa na nyaya za umeme lakini huduma hii ya umeme haijasambazwa katika maeneo mengi yanayotoa huduma za jamii. Ni nini tamko la Serikali kuhusiana na kupeleka umeme na kwa muda gani?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE):** Mheshimiwa Naibu Spika, kama ambavyo aliuliza kwenye swali la msingi, hasa alichotaka kujua ni kama kuna mpango wowote wa kupeleka umeme katika kituo cha afya cha Upuge na hii nimehakikisha kabisa kwamba tunapeleka umeme Upuge.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na Kata ya Ikongolo na Vijiji vya Kanyenye na Majengo sasa hivi tunaandaa *phase* ya tatu ya mpango wa kupeleka umeme vijijini. Tutajaribu katika mpango huo basi tuweze kuviweka vijiji hivi ili tuweze kutekeleza miradi hii kwenye mwaka 2014/2015.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili amesema juu ya maeneo ambayo yamepitiwa na nyaya zinazosafirisha umeme. Tunayo *program* ya *underline transformer,* kwenye maeneo yote yale ambayo umeme umepita tuweze kuweka *transformer* na tuweze kuwasambazia wananchi umeme, na hii tutaifanya kadiri ambavyo tutakuwa tunafanikiwa kupata fedha kwa sababu kazi yake si kubwa maana umeme upo ni kuweka *transformer* na kuwasambazia wananchi. Tutajitahidi kufanya hivyo kadiri tutakavyoweza kupata fedha.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, mkitazama muda wetu ni *almost* umeisha na nina maswali manne hapa. Kwa hiyo, ninawaomba radhi. Mheshimiwa Faith Mitambo, Mbunge wa Liwale, swali kutoka Makunjiganga.

Na. 463

**Upungufu kwenye Sheria ya Madini**

**MHE. FAITH M. MITAMBO** aliuliza:-

Sheria za Madini zilizopo sasa zinawanyima fursa na haki wamiliki wa maeneo husika kumiliki na kuchimba madini yanapogundulika kwenye maeneo yao wanayomiliki kisheria:-

(a) Je, kwa nini Serikali hairekebishi sheria hizo ili wamiliki wa maeneo husika yanayogundulika kuwa na rasilimali za Madini wawe na haki ya kumiliki au kuwa na *shares* na mtu mwingine atakayeruhusiwa kuchimba madini kweneye eneo hilo?

(b) Inapotokea mahali paligundulika kuwa na madini tayari pana miradi ya kudumu kama hospitali, shule na miradi mingine mikubwa ya uchimbaji inatakiwa kuchimba madini kwenye maeneo hayo Je, Serikali inasema nini juu ya fidia kwa wamiliki wenye taasisi hizo?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. STEPHEN J. MASELE)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini naomba kujibu swali la Mheshimiwa Faith Mohamed Mitambo, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria ya Madini ya Mwaka 2010 imetoa fursa kwa wazawa na wageni kumiliki leseni za aina mbalimbali, zikiwemo za utafiti *(PL),* uchimbaji

wa kati, *(ML),* uchimbaji wa mkubwa *(SML)* na uchimbaji mdogo *(PML)* kwa ajili ya wawekezaji wa ndani na nje kufanya shughuli za madini bila ubaguzi. Hata hivyo, umiliki wa leseni hizi haumpi mtu au kampuni kumiliki ardhi mpaka akidhi masharti ya kifungu Na. 95 cha Sheria ya Madini ya Mwaka 2010 na Sheria ya Ardhi Namba 4 ya Mwaka 1999.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ilirekebisha sera ya madini 1997 na sheria ya madini ya mwaka 1998 na kupata sera ya madini ya mwaka 2009 na Sheria ya Madini ya Mwaka 2010. Mabadiliko haya yanatokana na dhamira ya dhati ya Mheshimiwa Rais Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, ya kuainisha na kuondoa na kuboresha mapungufu yaliyokuwepo katika sera na sheria ya awali ikiwemo suala la mikataba na kuunda Tume ya Jaji Mark Bomani ya mwaka 2008. Serikali itaendelea kufanya marekebisho kadiri itakavyohitajika kwa kushirikiana na wadau.

Aidha, kifungu cha 95 cha Sheria ya Madini ya Mwaka 2010 kinamzuia mmiliki wa leseni ya madini kuanza kuchimba bila kupata ridhaa ya mmiliki wa ardhi.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu cha 95 cha Sheria ya Madini ya Mwaka 2010 kinatoa mwongozo kwa mmiliki yeyote wa leseni za madini kuomba na kupata ridhaa ya mmiliki halali wa ardhi kabla ya kuanza shughuli za utafutaji uchimbaji madini.

Kwa mujibu wa kifungu hicho na kwa mujibu wa Sheria ya Ardhi, Na. 4 ya mwaka 1999 kama ilivyofanyiwa marekebisho kwa nyakati mbalimbali, mmiliki halali wa ardhi anastahili fidia ili kupisha shughuli za uchimbaji pale itakapoonekana kuna ulazima wa kufanya hivyo.

Baadhi ya sehemu zilizopata fidia baada ya kufanyiwa tathmini kwa mujibu wa Sheria ya Ardhi (1999) ni pamoja na Tarime (maeneo ya Nyamongo na Nyabigena), Buzwagi (maeneo ya Mwime na Mwendakulima) na Geita (maeneo ya Katoma na Nyakabare). *(Makofi)*

**MHE. FAITH M. MITAMBO:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Spika. Mheshimiwa Naibu Waziri, kumekuwa na mkanganyiko wa kati ya Sheria ya Madini ya mwaka 2010 na Sheria za Ardhi. Hivyo kufanya viongozi wa ngazi za Serikali za Vijiji kutoa vibali na kuwaruhusu wachimbaji kuchimba na kufanya shughuli za machimbo bila kufuata taratibu. Je, Serikali ipo tayari kufafanua mkanganyiko huu wa Sheria ya Madini inayogongana na Sheria ya Ardhi?

Swali la pili, je ni taratibu kuwaruhusu wachimbaji wadogo wadogo na wakubwa kufanya shughuli zao za uchimbaji katika maeneo ambayo tayari yana leseni ya *PML, ML, SML* na *PL? (Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. STEPHEN J. MASELE):** Mheshimiwa Naibu Spika, hakuna mkanganyiko wowote katika Sheria ya Ardhi kama nilivyoieleza Sheria Na. 4 ya Mwaka 1999 na Sheria ya Madini ya Mwaka 2010.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukitazama katika Sheria ya Ardhi, Sura 113 hasa kipengele Na. 2 ambacho kinazungumzia tafsiri ya ardhi. Inasema wazi ardhi ni sura ya nchi sehemu ambayo ni sura ya dunia na inaeleza kabisa kwamba ardhi ni pamoja na vitu vilivyopo chini ya ardhi. Lakini isipokuwa madini na mafuta. Sasa ukiangalia Mheshimiwa Mbunge anachooeleza hapa ni mkanganyiko wa nani anamiliki kule chini ya ardhi. Lakini Kifungu Na. 4 cha Sheria hiyo hiyo ya Ardhi inaeleza kabisa kwamba Rais ndiyo *trustee* ama *superior land lord* ambaye ndiye anayesimamia ardhi kwa niaba ya Watanzania wote na sisi Watanzania ikiwemo Waheshimiwa Wabunge humu ni wapangaji tu na tunapanga hivyo kupitia *Title Deed* zetu ambazo tunalipia kwa miaka 33 na miaka 99 na kila mwaka tunalipa hiyo *land rent.*

Kwa misingi hiyo sasa Sheria ya Madini hasa Kifungu Na. 35 ambacho kinampa haki mmiliki yoyote wa leseni hasa leseni ya utafiti kufanya shughuli zake za leseni za utafiti. Lakini hakimmilikishi ardhi ile kama nilivyoeleza hapa kwenye Sura hii na tafsiri ya Sheria ya Ardhi.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Naibu Spika, hakuna mkanganyiko bali Sheria hizi zote zinafanya kazi kwa pamoja na Sheria hizi ni lazima zizingatie Sheria nyingine. Kwa hiyo, Sheria ya Ardhi izingatie Sheria ya Madini na Sheria ya Madini izingatie Sheria ya Ardhi.

Na. 464

**Kampuni Ndogo Kutumia Soko la Mitaji**

**MHE. DIANA M. CHILOLO K.n.y. (MHE. DEVOTA M. LIKOKOLA)** aliuliza:-

(a) Je, Serikali itakuwa tayari kuhamasisha wananchi wenye kampuni ndogo kutumia soko la mitaji ili kuondokana na tatizo la mitaji?

(b) Je, ni kwa jinsi gani Serikali itatekeleza jambo hilo?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. SAADA M. SALUM)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Devota Likokola, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana *(Capital Markets Structure and Securities Authority (CMSA),* ilifanya utafiti mwaka 2006 ili kubaini mapungufu na kupata mapendekezo ya namna ya kuzishirikisha kampuni ndogo na za kati kushiriki kwenye soko la mitaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, moja ya mapendekezo ya utafiti huo ilikuwa ni kuanzishwa kwa safu nyingine mbadala kwenye soko la Hisa la Dar es Salaam itakayohusika na uorodheshwaji wa kampuni ndogo na za kati zisizo na historia ya utendaji na ambazo haziwezi kukidhi vigezo na masharti ya safu kuu ya soko la hisa yaani *(Main Investment Market Segment)*.

Kwa kuzingatia mapendekezo haya, Serikali imechukua hatua ya kulegeza masharti na vigezo vya kuorodheshwa kwenye soko la Hisa. Madhumuni ya hatua hii ni kukuza ujasiriamali na kuziwezesha kampuni changa, ndogo na za kati kushiriki kwenye soko la Mitaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali pia imefanya marekebisho ya kanuni za kusimamia soko la Mitaji ili ziweze kutumiwa na kampuni ndogo na za kati. Taratibu za Soko la Hisa la Dar es Salaam nazo pia zilibadilishwa ili kuruhusu kuorodheshwa, kuuzwa na kununuliwa kwa hisa za kampuni ndogo na za kati. Aidha, zoezi hili lilijumuisha kutengeneza kanuni maalum za usajili wa wataalam kwa ajilii ya kuzilea na kuzishauri kampuni zinazotarajia kuorodheshwa kwenye soko la kukuzia ujasiriamali.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maandalizi kukamilika, *CMSA* ilitoa matangazo kwenye vyombo vya habari ili kuzishawishi kampuni za kutoa ushauri elekezi kutuma maombi ya usajili kwa Mamlaka, yaani *CMSA.* Hadi kufikia sasa, ni kampuni nne za wataalam washauri zimejitokeza na kusajiliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kwa kushirikiana na CMSA itaendelea kutoa elimu ya kuhamasisha wananchi wenye kampuni ndogo na kati kutumia fursa za soko la mitaji ili kujipatia mitaji kwa ajili ya kuendesha shughuli zao za kiuchumi.

Vile vile, *CMSA* kwa kushirikiana na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi wanaangalia namna ambavyo elimu kuhusu masoko ya mitaji inaweza kuingizwa kwenye Mitaala ya Vyuo na Shule za Sekondari ili kupanua wigo wa elimu ya masoko ya mitaji na dhamana hapa nchini. *(Makofi)*

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, napenda kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza.

La kwanza, ili uweze kunufaika na soko la hisa ni kununua hisa na kuuza hisa pale zitakapopanda bei. Kwa kuwa hisa zinapopanda bei wateja huwa siyo rahisi kupata taarifa wakiwemo Waheshimiwa Wabunge wengi wamenunua hisa.

Je, Serikali itakuwa tayari sasa kutoa taarifa kwa wateja kwa maandishi ili zinapopanda bei wateja waweze kuuza hisa kwa lengo la kunufaika na soko hili la hisa?

Swali la pili. Kwa kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri amekiri kwamba sasa masharti ya soko la mitaji yamelegezwa. Na kwa kuwa kampuni ndogo na za kati sasa ziko nyingi mikoani na Ofisi hii iko Dar es Salaam tu.

Je, Serikali itakuwa tayari kufungua Ofisi hata Ofisi za Kanda ili kampuni ndogo na za kati ziweze kunufaika kukopa kwenye soko hili la mitaji? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. SAADA M. SALUM):** Mheshimiwa Naibu Spika, kikawaida *CMSA* na *Dar es Salaam Stock Exchange* inakuwa inatoa taarifa zake hususan katika vyombo vya habari kawaida wanatazama kampuni zenyewe zinakuwa zinatangaza ule mwenendo wa shares, *share prices*.

Sasa tukiangalia kwa wale ambao watakuwa na elimu hasa ya *finance* pamoja na *Capital Market Structure* watakuwa wanafuatilia ule mwenendo hasa hususan kwenye taarifa za habari walikuwa wakati wa ile *statement* ya biashara na uchumi wanakuwa wanatoa hizi taarifa *of course* kwa mtu wa kawaida ambaye atakuwa hana elimu atakuwa hajui *the work of DSE* hatafahamu.

Lakini hata hivyo tumeshazungumza na *Dar es Salaam Stock Exchange* kuanza sasa kutoa elimu kwa njia rahisi kwa lugha nyepesi kabisa ili mwananchi tu wa kawaida ambaye ana fedha zake lakini hajui wapi pa kwenda kuzipeleka awe naye anafahamu kwamba kuna hili soko la hisa ambako

anaweza kwenda kuuza, anaweza kwenda kununua *shares* na yeye akawa mmiliki wa hizi kampuni. Kwa hivyo hilo tunaangalia mikakati ili ya kuweza kuhamasisha zaidi kwa kutoa elimu.

Lakini kuhusu kufungua hizi Taasisi hizi za masoko katika mikoa mingine. Kwa kuanzia tumeanza na Dar es Salaam kweli kwa sababu ni mji ambao ni mkubwa unakuwa sana kibiashara. Lakini kuna *intention* ya kwenda katika Mikoa mingine. Kwa sababu ku-*manage Stock Exchange* ni kazi ambayo inahitaji weledi na inahitaji taaluma kubwa sana na inahitaji vile vile teknolojia kubwa sana na teknolojia inakuwa inabadilika badilika.

Kwa hivyo kwa sasa tuko Dar es Salaam lakini *intention* yetu hasa ni kwenda katika Mikoa mingine ili wananchi ambao wapo katika hiyo mikoa mingine wapate fursa na wao kuwekeza na kuwa wamiliki katika makampuni hayo. Ahsante sana. *(Makofi)*

Na. 465

**Biashara ya Kubadilisha Fedha Nchini**

**MHE. MARGARETH A. MKANGA** aliuliza:-

Je, Serikali inadhibiti vipi mwenendo wa biashara katika maduka ya kubadilisha fedha yaliyoko nchini kwa sasa?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. JANET ZEBEDAYO MBENE)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Margareth Agnes Mkanga, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, maduka yote ya kubadilishia fedha za kigeni yanaendeshwa kwa mujibu wa kanuni za maduka ya kubadiilshia fedha za kigeni ya mwaka

2008, yaani *The foreign Exchange Bureau De Change, Regulations 2008.* Kanuni hizo ziliwekwa kwa mujibu wa ibara ya 5(a) na 7(1) ya Sheria ya Fedha za Kigeni ya mwaka 1992 inayompa mamlaka Gavana wa Benki Kuu ya kusimamia maduka ya kubadilisha fedha za kigeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, chini ya vifungu vya kanuni hizi, maduka yote ya kubadilisha fedha za kigeni lazima yaanzishwe kama kampuni; yamilikiwe na kuendeshwa na Watanzania, yaanze na mtaji usiopungua shilingi 40,000,000/=; hayaruhusiwi kusafirisha fedha nje ya nchi, yanatakiwa kuweka kumbukumbu ya mauzo na manunuzi kwenye nukushi yaani *(computer)* na kutoa stakabadhi inayochapishwa kutoka kwenye nukushi inayoonesha muda wa mauzo au manunuzi ya fedha; yanatakiwa kuwasilisha taarifa za bei za kuuza na kununua fedha za kigeni kila siku na kila mwezi; na mwisho, yanatakiwa kuwasilisha hesabu zilizokaguliwa kila mwisho wa mwaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kukabiliana na matatizo mbalimbali yanayojitokeza, Benki Kuu inafanya yafuatayo:-

Kwa maombi mapya ya leseni, waombaji wanatakiwa kuleta maelezo yao binafsi *(CV),* Vyanzo vya mitaji yao, pamoja na rekodi ya malipo ya kodi kwa kipindi cha miaka mitatu. Hutoa mafunzo ya kanuni za uendeshaji wa maduka ya uuzaji na ununuzi wa fedha za kigeni na kuwafanyia usaili Wakurugenzi na Waendeshaji waandamizi kabla ya kutoa leseni mpya; huongeza muda wa leseni baada ya kujiridhisha kuwa duka husika limetimiza kanuni za uendeshaji. Pia, Benki Kuu hutoa elimu kwa umma kuhusu umuhimu wa kudai stakabadhi za ununuzi na uuzaji wa fedha za kigeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakaguzi wa mabenki hupitia maduka yote kuangalia na kusimamia utekelezaji wa kanuni za kuendesha maduka ya kubadilisha fedha za kigeni.

Aidha, wanaokiuka kanuni hupewa adhabu zifuatazo:- hupewa onyo kali; hulipa faini isiyopungua shilingi 2,500,000/=; hufungiwa biashara kwa muda wa miezi 3 hadi 6; na mwisho, hunyang'anywa leseni kwa mujibu wa Sheria.

**MHE. MARGARETH A. MKANGA:** Nashukuru Mheshimiwa Naibu Spika kwa kunipa nafasi. Kwa vile tatizo la kupewa stakabadhi unaponunua au unapouziwa imekuwa ni kubwa hapa nchini.

Je, Serikali ina uhakika gani wa komputa za kutoa stakabadhi hizi hasa kwa zile Taasisi au Kampuni za kubadilisha fedha zilizoanza mwanzoni kabla ya utaratibu huu?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. JANET Z. MBENE):** Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ina uhakika wa hizo *computer* ambazo zimewekwa kwenye Bureau kwa sababu zinakaguliwa mara kwa mara. Kuna Kitengo Maalum cha Benki Kuu ambacho kinafanya kazi ya kukagua mabenki pamoja na taasisi zote zinazojihusisha na masuala ya kifedha. Kwa hiyo, nina uhakika wa hizi *computer* upo. Suala la kudai risiti kwa kweli ni suala la wananchi husika wanapokwenda kwenye maduka ya kubadilisha fedha kwenye maduka kununua bidhaa mbalimbali, huduma mbali mbali ni wajibu wetu sisi sote kudai hizi risiti. Lakini vile vile na sisi tunapokwenda kwenye *Bureau De Change* twende na vitambulisho vyetu kama *Passport* na nyaraka zinazohitajika ili waweze kuziingiza katika kompyuta hizi kwa ajili ya kuweka kumbukumbu sahihi. *(Makofi)*

Na. 466

**Lugha za Matusi kwa Watumiaji wa Simu**

**MHE. LOLESIA J. BUKWIMBA K.n.y. (MHE. MCH. DKT. GETRUDE P. RWAKATARE)** aliuliza:-

Mamlaka ya Mawasiliano nchini *(TCRA)* ilifanya zoezi la kusajili na kuorodhesha namba za watumiaji wa simu za

mikononi kwa madhumuni ya kudhibiti matumizi sahihi na usalama kwa watumiaji wa simu lakini bado kuna baadhi ya watu hutumia simu hizo kusambaza ujumbe mfupi (SMS) na maneno ya kuzusha:-

Je, Serikali inasema nini juu ya tatizo hilo?

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Getrude Rwakatare, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kuwa Wizara kupitia Mamlaka ya Mawasiliano nchini *TCRA* ilifanya zoezi la kusajili namba za watumiaji wa simu za mikononi ambapo hadi sasa namba za simu milioni ishirini na nne mia nne na tatu elfu mia sita tisini na tisa zimesajiliwa. Usajili huu wa namba pamoja na mambo mengine, ulikuwa na lengo la kupunguza matumizi mabaya ya simu za mikononi.

Mheshimiwa Naibu Spika, usajili wa namba za simu ulikuwa ni hatua muhimu ya utekelezaji wa dhamira ya Serikali kuzuia matumizi mabaya ya simu hizo. Hata hivyo, changamoto kadhaa zilijitokeza na kuendelea kuwepo kwa matumizi mabaya ya simu. Changamoto hizo ni kama ifuatavyo:-

(i) Muda uliokuwa ukitolewa wa siku 30 wa kusajili simu, hivyo watu kupata mwanya wa kuzitumia simu hizo vibaya katika kipindi hicho ambacho siku 30 ambazo tulizitoa kama siku za msamaha.

(ii) Vile vile baadhi ya Mawakala wa kusajili simu walisajili simu hizo bila vitambulisho au kwa majina halisi ya watumiaji.

(iii) Vile vile kutokuwepo kwa vitambulisho vya taifa ambavyo vingeweza kuhakiki majina halisi ya mtumiaji ilikuwa ni changamoto nyingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali katika kukabiliana na matumizi mabaya ya simu, imefanya mambo yafuatayo:-

(i) Tumekamilisha Kanuni za Sheria ya Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta *(EPOCA)* zitakazodhibiti matumizi mabaya ya simu.

(ii) Vile vile tumeondoa siku 30 kipindi ambacho mtu alikua akiweza kutumia simu bila kujisajili kipindi hicho sasa hakitakuwepo.

(iii) Vile vile tumeamua kuzima simu zote ambazo hazijasaliwa ifikapo tarehe 10 Julai, 2013.

(iv) Vile vile kama Serikali tumeendelea kukamilisha zoezi la upatikanaji wa vitambulisho vya taifa kama njia muhimu ya kuhakiki watumiaji halisi wa simu hizi.

(v) Vile vile tutashirikiana na jeshi la polisi katika kuwasaka na kuwakamata wale wote wanaotumia simu vibaya.

**MHE. LOLESIA J. BUKWIMBA:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Naibu Spika kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwanza nishukuru kwa majibu ya Serikali. Lakini pamoja na majibu hayo Serikali imekiri kabisa kwamba tatizo bado lipo. Bado matumizi mabaya ya simu yapo. Changamoto ambazo Serikali imezitaja ni pamoja na Mawakala kutokutumia vitambulisho wakati wa kusajili hizi simu *card.* Vile vile kutokuwepo kwa vitambulisho vya kitaifa. Sasa ningependa kujua swali la kwanza:-

Serikali inatoa kauli gani kwa Mawakala ambao wanasajili simu *card* bila ya kutumia vitambulisho?

Swali la pili. Kwa kuwa vitambulisho vya kitaifa ni muhimu sana. Ningependa kujua sasa ni lini Serikali itatoa vitambulisho hivi kwa Watanzania wote? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Sijui kama hili la mwisho ataliweza? Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa yale ambayo una ubavu nayo, majibu?

**NAIBU WAZIRI WA SAYANSI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia, napenda kujibu swali moja la nyongeza la Mheshimiwa Lolesia Bukwimba, Mbunge wa Busanda, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi ya kusajili watumiaji ilikuwa ni kazi ya makampuni ya simu, uamuzi ulikuwa ni wa Serikali, lakini tuliwapa shughuli hiyo wenzetu makampuni ya simu kwamba, kwa wale wanaoenda kupata *sim card* mpya na wale waliokuwa na *sim card* za zamani, basi wenzetu wataweka utaratibu wa kuwasajili.

Lakini bahati mbaya, kama nilivyosema awali kumejitokeza tatizo la kutokuwepo na uaminifu kwa wale waliopewa kazi ya kusajili kwamba, inawezekana kabisa ukaenda pale kwenye meza ya kusajili ukasema umesahau kitambulisho, lakini mimi naitwa Juma Athumani na ukasajiliwa hivyo. Tulichogundua ni kwamba, kumekuwa na majina *fake* kwamba, simu imesajiliwa kabisa lakini jina lililoandikwa ni *fake* na watu wengi wanatumia simu hizo kufanya uhalifu, kueneza *message* za uchochezi pamoja na matusi na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ambacho tumefanya ni kwanza, tumeimarisha Kanuni za Sheria hii ili kutoa adhabu zaidi inapobainika kwamba, hakukuwa na uamini fu katika usajili. Lakini pili, kama nilivyosema, ni hili suala la vitambulisho vya taifa kwamba, itakapofika sasa kila mtu amepata kitambulisho cha Taifa tutafanya uhakiki upya wa zoezi hili, ili kila aliye na *sim card* basi, simu ile iwe imesajiliwa kwenye jina lake halisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, jingine la kuongeza tu ni kwamba, Mwanasheria Mkuu hapa atakubali kwamba, Sheria ni jambo moja, lakini Sheria zinafanya kazi katika utamaduni wa kwenye jamii. Tunafahamu kwamba, na ulitokea mfano Mheshimiwa Naibu Spika na wewe ulikuwa ni *victim* kwamba, wapo wenzetu walienda kwenye jukwaa wakatangaza namba za Viongozi ili watu wawatumie *message.* Na ile haikatazwi Kisheria, kinachokatazwa Kisheria ni yule anayetuma *message* sasa kutumia vibaya ile simu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, mategemeo yetu ni kwamba, sisi pamoja na kwamba, haikatazwi Kisheria mtu ku-*share* namba ya mtu mwingine, wenzetu wangekuwa na ustaarabu wa kutofanya hivyo. Kwamba, pamoja na kwamba, huvunji Sheria, lakini kuna misingi ya ustaarabu kwenye jamii. Kwa hiyo, baadhi ya vitu vina-*reflect* zaidi ustaarabu wa watu kuliko uimara wa Sheria zetu. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nawashukuruni sana kwa ushirikiano wenu katika kipindi hiki cha Maswali. Maswali yamekamilika, ninayo Matangazo machache, naomba masikio yenu, tuanze na Wageni.

Kwanza nimkaribishe sana Mheshimiwa Moses Machali, Mbunge mwenzetu, ambaye sasa ameweza kuwasili humu Bungeni, tuko na yeye humu ndani baada ya kupata matatizo yale aliyoyapata. Tunaishukuru sana Serikali, kwa ushirikiano ambao mmempa, mkubwa sana. Na tunakupa pole Wabunge wote kwa yale yote yaliyokupata; tunaamini kabisa mguu wako utazidi kupata nafuu. Karibu sana Mheshimiwa Machali. *(Makofi)*

Lakini pia niwakaribishe Bungeni Wabunge ambao hawakuwepo; nimkaribishe Mheshimiwa Joyce Mukya, ni muda mrefu sana hakuwepo. Karibu sana Bungeni. Tunataka kumwona mjomba wetu, karibu sana Joyce. *(Makofi)*

Wageni wengine walioko Bungeni, ni pamoja na wanafunzi waliokuja kujifunza kutoka shule ya Viganga – Kongwa. Pale mlipo, wale Walimu na wanafunzi wa Viganga – Kongwa? Karibuni sana, pale kwenye kona, karibuni sana sana Walimu wangu na wanangu. *(Makofi)*

Wanafunzi 50 na Walimu wao kutoka Shule ya Msingi ya Sokoine Dodoma? Karibuni sana Wanafunzi na Walimu wa Sokoine Dodoma, karibuni sana. *(Makofi)*

Wanafunzi 60 na Walimu wao kutoka *PCEA Saint Columbia Nursery and Primary Schools* za Dar-es-Salaam. Karibuni sana, watoto wazuri jamani. Karibuni sana Walimu na Wanafunzi. *(Makofi)*

Wanafunzi na Walimu wao na Mwenyekiti wa Bodi kutoka Shule ya Sekondari Kimagai – Mpwapwa, ambao ni Wageni wa Mheshimiwa Gregory Teu. Ahsanteni sana Wanafunzi wa kutoka Kimagai; kwa Kigogo inabidi iitwe "Chimagai," karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni 16 ambao ni Makatibu wa kutoka Jimbo la Tabora Kaskazini, wageni wa Mheshimiwa Shaffin Abdallah. Karibuni sana Wanyamwezi wote kutoka Tabora Kaskazini. Muwe makini tu, Dodoma magari ni mengi kuliko Tabora hasa, mnapokatiza barabara. *(Makofi)*

Wageni 28 ambao ni Madiwani kutoka Baraza la Madiwani la Halmashauri ya Wilaya ya Kilolo – Iringa, ambao ni wageni wa Mheshimiwa Profesa Peter Msolla. Ahsanteni sana Waheshimiwa Madiwani na kwa hatua hii niwapongeze sana Mabaraza ya Madiwani ambayo yametutembelea hapa Bungeni katika kipindi chote cha Bajeti na nitoe wito kwa Waheshimiwa Madiwani wengine wa Halmashauri nyingine, wanapopata nafasi kutembelea Bunge na kujifunza na kuona namna ambavyo Bunge linafanya kazi kwa sababu, kazi zao kwa sehemu kubwa zinaendana na namna Bunge linafanya kazi. *(Makofi)*

Kwa hiyo, kwa Madiwani walio wengi nchi nzima Bunge, ni mahali pa kujifunza mambo mengi yanayohusu kazi zao. Tunawakaribisha sana. *(Makofi)*

Kuna wageni wa Mheshimiwa Naibu Waziri Makongoro Mahanga wageni 112 kutoka *Sherehe Arts Association,* pale Mlipo? Karibuni sana, wengi wa hawa Waheshimiwa Wabunge, ni "Washehereshaji," Ma-*MC* na watu wa namna hiyo. Karibu sana na miongoni mwao wako wageni wa Mheshimiwa Sitta, Bwana Joshua Malembeka, Nesta na Doris, tunawakaribisha sana, karibuni sana. *(Makofi)*

Matangazo ya Kazi; Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji, Mheshimiwa Prof. Peter Msolla, Profesa Msolla, anawaomba Wajumbe wa Kamati hiyo, tutakapomaliza shughuli zetu asubuhi hii basi wakutane Ukumbi Namba 227. Muda si mrefu tutamaliza shughuli zetu, tutakapomaliza Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji mkutane Ukumbi 227, Jengo la Utawala.

Mheshimiwa Jenista Mhagama, Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii, anawaomba Wajumbe wa Kamati yake ya Maendeleo ya Jamii, mkutane tutakapomaliza mambo yetu hapa, Msekwa *C.*

Mheshimiwa Victor Mwambalaswa, Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Nishati na Madini, anawaomba Wajumbe wa Kamati ya Nishati na Madini Mkutane tutakapomaliza mambo yetu haya katika Ukumbi wa Msekwa, kwa ujumla wake.

Mheshimiwa Pindi Chana, Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala, anawaomba Wajumbe wa Kamati hiyo, mara baada ya shughuli zinazoendelea hivi sasa zikimalizika, basi wakutane Ukumbi wa *Basement.* Kamati ya Mheshimiwa Pindi Chana, ya Katiba, Sheria na Utawala tutakapomaliza tu basi wakutane *Basement.*

Mwisho kuna wale wazee wetu 30 kutoka Butiama, sijui wamekaa upande gani? Karibuni sana, karibuni sana; mtupelekee salaam zetu kwa Mama Maria huko Butiama. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, nawaomba mwendelee na uvumilivu kidogo. Kuna Kauli fupi mbili (2) zinafuata naomba tuzisikilize, baada ya mambo hayo tutakuwa tumefika mahali pazuri, nitawapa maelekezo fulani, lakini tutamaliza mapema sana, nawaahidi leo. *(Makofi)*

Katibu tuendelee?

## KAULI ZA MAWAZIRI

### Ajali Zinazotokana na Matumizi ya Pikipiki

**NAIBU SPIKA:** Kauli za Mawaziri. Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 49 (1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Aprili, 2013, naomba kuwasilisha Taarifa kuhusu ajali za barabarani zinazotokana na matumizi ya pikipiki nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, matatizo ya ajira kwa vijana, usafiri na usafirishaji nchini ulifanya Serikali, ikubali kuidhinisha pikipiki za matairi 2 na matairi 3, maarufu kama Bajaji, kutumika katika biashara ya usafiri na usafirishaji wa abiria nchini. Uamuzi huu ulifanywa ili kuongeza wigo wa ajira kwa vijana, ili kuwapa uwezo wa kupata kipato kwa kazi halali.

Mheshimiwa Naibu Spika, sote ni mashahidi wa namna uamuzi huu ulivyosaidia kwa kiasi kikubwa kuwapatia vijana wengi nchini shughuli ya kuwapatia kipato halali na kuwaepusha na uwezekano wa kushawishika kujiingiza katika shughuli haramu, ikiwemo uhalifu.

Pamoja na kutoa ajira kwa vijana, uamuzi huu wa Serikali, pia umesaidia kupunguza kwa kiasi kikubwa tatizo la usafiri katika maeneo mengi nchini, hasa katika maeneo ambayo usafiri wa magari wa uhakika haupo.

Maeneo mengi ambayo magari ya abiria hayawezi kufika sasa, yanafikika kirahisi kwa pikiki. Wananchi wa kipato cha chini wanaweza kutoka eneo moja kwenda jingine kwa gharama nafuu, tofauti na hali ilivyokuwa kabla ya uamuzi huo wa Serikali.

Aidha, katika miji mingi yenye msongamano mkubwa wa magari barabarani, hususan Jiji la Dar-es-Salaam, pikipiki zinasaidia sana wananchi kuepuka msongamano na kuwahi katika shughuli zao za kujipatia kipato na kurejea majumbani kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama ambavyo mambo mengi mema siku zote hayakosi changamoto, matumizi ya pikipiki katika usafirishaji wa abiria yanakabiliwa na changamoto mbalimbali, ambapo kubwa kuliko zote ni ajali nyingi za barabarani zinazohusisha pikipiki.

Matumizi ya pikipiki nchini yamesababisha ongezeko kubwa sana la ajaili za barabarani ambazo zimegharimu maisha ya watanzania wenzetu wengi sana. Pamoja na upotevu wa maisha, ajali hizi zimesababisha ulemavu wa kudumu kwa watu wengi na kupoteza viungo vyao na kuwafanya wawe tegemezi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa takwimu za Jeshi la Polisi Nchini, katika kipindi cha kuanzia Januari 2012 hadi kufikia mwezi Mei, 2013 idadi ya pikipiki zilizosajiliwa nchi nzima ilikuwa 10,036. Mikoa inayoongoza kwa wingi wa pikipiki kwa mujibu wa takwimu hizi ni Jiji la Dar-es-Salaam lenye jumla ya pikipiki 2,024; katika idadi hiyo ya pikipiki Kinondoni ina jumla ya pikipiki 1,735 Temeke 1,363 Ilala 1,334. Mikoa inayofuatia kwa idadi kubwa ya pikipiki ni Morogoro, Arusha na Kilimanjaro.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha Januri hadi Disemba 2012 kulitokea jumla ya ajali 5,763 ambazo zimegharimu maisha ya Watanzania 930, naomba kurudia; katika kipindi cha Januari hadi Disemba 2013, Januari hadi Disemba 2013 kulitokea jumla ya ajali 5,763 ambazo zimegharimu maisha ya Watanzania 930 na kuwajeruhi wengine 5,532. Mkoa wa Dar-es-Salaam, uliongoza kwa kuwa na ajali 2,479 ambapo Wilaya ya Kinondoni ilikuwa na ajli 1,007 Temeke 769, Ilala 703.

Ajali hizi zimesababisha vifo 164 na majeruhi 2,765 idadi hii ni kubwa sana. Mikoa inayofuatia kwa ajali ni Arusha, iliyokuwa na ajali 569 zilizosababisha vifo 65 na majeruhi 420. Mkoa wa Morogoro ulikuwa na ajali 431 zilizosababisha vifo 54 na majeruhi 328 na Kilimanjaro ilikuwa na ajali 294 zilizosababisha vifo 52 na majeru 266.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha Januari hadi Mei, 2013, takwimu zinaonesha kuwa kumetokea ajali za pikipiki 2,415 nchi nzima. Ajali hizo zimesababisha watu 352 kupoteza maisha yao na wengine 2,368 kujeruhiwa.

Mkoa wa Dar-es-Salaam umeongeza kwa matukio ya ajali 2,161 zilizosababisha vifo 56 na majeruhi 1,211 kwa mchanganuo ufuatao; Wilaya ya Kinondoni ajali 515, vifo 22, majeruhi 549. Temeke ajali 269, vifo 19 na majeruhi 354 na Ilala ajali 357, vifo 15, majeruhi 307. Takwimu za Mikoa mingine inayoongoza kwa ajali ni Mkoa wa Morogoro uliokuwa na ajali 186 zilizosababisha vifo 15 na majeruhi 117. Arusha ajali 118, vifo 16 na majeruhi 102; Kilimanjaro ajali 130, vifo 36, majeruhi 120. Mkoa wa Pwani, ajali 114 zilizosababisha vifo 23 na majeruhi 167.

Mheshimiwa Naibu Spika, matukio ya ajali za pikipiki ni mengi na kwa mujibu wa takwimu nilizozitaja hapo juu, idadi ya vifo na majeruhi ni kubwa kwa kiasi cha kusababisha Hospitali nyingi nchini kuanzisha Wodi maalum za majeruhi wa pikipiki.

Tusipochukua hatua za makusudi, Taifa letu litaendelea kuathirika na ajali hizo ambazo zinachukua maisha ya watu wetu na kuongeza idadi ya yatima, walemavu na watu wasiojiweza na kuwafanya wawe tegemezi.

Mheshimiwa Naibu Spika, vyanzo vikuu vya ajali za barabarani zinazohusisha pikipiki ni pamoja na kutokujua Sheria, Kanuni na Taratibu za matumizi ya barabara, ambapo madereva wengi wa pikipiki hawana leseni za udereva. Uendeshaji wa hatari wa pikipiki barabarani kwa mwendo kasi na kupita magari mengine bila sababu, kupita katika taa za kuongozea magari *(Traffic Lights)* bila kuruhusiwa, kudharau Askari wa Usalama Barabarani wanaoongoza magari katika makutano ya barabara, kupakiza abiria watatu au zaidi katika pikipiki moja, maarufu kama mshikaki, na matumizi ya ulevi kwa waendeshaji wa pikipiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, sababu nyingine ni miundombinu ya barabara ambapo baadhi ya barabara zinakosa alama au zinakuwa na alama zilizofifia ambazo sio rahisi kuonekana. Barabara kutumika na makundi yote ya watumiaji *(Traffic Mix),* ambapo magari, baiskeli, pikipiki, mikokoteni na watembea kwa miguu pamoja na ubovu wa barabara, wote hutumia njia moja. Madereva wa magari kutoheshimu wapanda pikipiki ni sababu nyingine inayosababisha ajali za pikipiki nchini.

Madereva wa magari mara nyingi wamekuwa hawatoi ushirikiano mzuri kwa madareva wa pikipiki, wanapokuwa barabarani. Tabia hii ya madereva wa magari inatokana na mtazamo hasi kuhusu waendesha pikipiki, ambapo watu wengi wanaamini kuwa waendesha pikipiki hawana nidhamu ya barabarani.

Mheshimiwa Naibu Spika, mikakati mbalimbali inafanywa na Jesho la Polisi katika kukabiliana na wimbi kubwa la ajali za pikipiki, ili kunusuru hali hii. Mikakati hiyo ni pamoja na usimamizi na udhibiti wa watoaji na watumiaji wa usafiri huo; usimamizi huu unafanywa kwa kutumia Kanuni

za *SUMATRA* za mwaka 2010 zinzohusu usafirishaji wa abiria kwa kutumia pikipiki. Waendesha pikipiki kutoa taarifa za uhalifu na makosa ya wanapoona wenzao wanakiuka taratibu.

Kuandaa *operations* mbalimbali kwa lengo la kuhakikisha kuwa waendeshaji wa pikipiki wanafuata Sheria katika uendeshaji, ni pamoja na kuwa leseni halali, upakiaji salama wa abiria, matumizi ya kofia ngumu *(Helmet)* na uendeshaji wa kujihami.

Mheshimiwa Naibu Spika, mikakati mingine ni pamoja na kutoa utoaji wa elimu kwa kutumia vyombo vya habari kama Redio, *Television* na Magazeti. Kuandaa vipeperushi vya elimu kwa waendesha pikipiki, kutoa mafunzo katika vituo mbalimbali vya waendesha pikipiki.

Mafunzo haya yanafanywa na Jeshi la Polisi kwa kushirikiana na Wadau mbalimbali kama asasi zisizo za Kiserikali na Vyuo vya Udereva Nchini, hususan *VETA.*

Mheshimiwa Naibu Spika, njia nyingine ya utoaji wa elimu ni kushirikisha waendesha pikipiki katika michezo. Katika maeneo mbalimbali nchini Jeshi la Polisi kwa kushirikiana na wadau na wadhamini wa michezo huandaa michezo mbalimbali inayowahusisha waendesha pikipiki na makundi mbalimbali ya watumiaji wa barabara. Wakuu wa Polisi wa Usalama Barabarani wa Mikoa, huandaa michezo hii na kutumia fursa hiyo, kutoa elimu ya usalama barabarani kwa waendesha pikipiki. Mfano wa michezo hiyo ni kombe la Mpinga *(Mpinga Cup)* lililofanyika katika Mkoa wa Kipolisi wa Kinondoni.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeanza kukuelezea uamuzi wa Serikali, kuhusu pikipiki kutumika katika usafirishaji wa abiria, faida zinazopatikana na changamoto kubwa zilizojitokeza kutokana na matumizi ya pikipiki katika usafirishaji. Idadi ya pikipiki nchini ni kubwa na inazidi kuongezeka kila siku.

Idadi ya ajali, vifo na majeruhi, nayo inazidi kuongezeka siku hadi siku kadiri pikipiki zinazvyoongezeka. Ukitazama takwimu nilizotoa awali utagundua kuwa upo uhusiano mkubwa kati ya idadi ya pikipiki na ajali zinazotokea.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa takwimu hizi ni wazi tunalo tatizo kubwa sana katika sekta ya usafirishaji wa abiria kwa kutumia pikipiki. Naomba nitumie fursa hii kwa kutumia Bunge lako Tukufu, kuwaomba Waheshimiwa Wabunge, wasaidie katika kuwahamasisha vijana, hasa madereva wa boda-boda kuhakikisha kuwa wanapata mafunzo ya udereva, kujifunza Sheria za usalama barabarani na kuziheshimu.

Kuepuka kuzidisha abiria, kuepuka kuvuka taa za kuongozea magari iwapo taa hazijawaruhusu kufanya hivyo, kuzingatia maelekezo ya Askari wa Usalama Barabarani wanaoongoza magari katika makutano ya barabara. Kutumia kofia ngumu zilizo na viwango kwa usalama wao na abiria wanaowasafirisha, badala ya kuvaa tu ili mradi wasibughudhiwe na Polisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, natoa wito kwa wananchi wote wanaotumia usafiri wa pikipiki, kutokubali kupanda pikipiki bila kuvaa kofia ngumu *(Helmet).* Kuwasisitiza mara kwa mara madereva waliowabeba kuendesha pikipiki kwa mwendo wa wastani. Kuwa makini na kufuata kikamilifu Sheria za Usalama Barabarani kwa usalama wao. Aidha, ninawaagiza Polisi wa Usalama Barabarani kuwadhibiti kwa mujibu wa Sheria na Kanuni zilizopo waendesha-pikipiki wakorofi wasiopenda kufuata Sheria za Usalama Barabarani bila kushurutishwa.

Kujiepusha na upendeleo, kujiepusha na rushwa katika kutekeleza wajibu wao na kusimamia kikamilifu mkakati wa Polisi Jamii katika eneo hili, ili kupunguza changamoto zinazoikabili sekta hii ya usafiri na usafirishaji wa abiria kwa kutumia pikipiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, jukumu la kupambana na changamoto hizi ni letu sote ni vema wadau wote washirikiane kwa pamoja kwa manufaa ya wananchi badala ya wengine kukaa pembeni na kutoa lawama kwa Serikali.

Iwapo tunakubaliana kuwa jambo hili lina maslahi kwetu na kwa wananchi wetu basi ni vema tuweke nguvu zetu pamoja ili kukabiliana na changamoto hizi.

Napenda kutahadharisha kuwa jeshi la polisi litakuwa makini na madhubuti katika kusimamia Sheria hivyo ni vyema kila muhusika afuate Sheria.

Kwa kufuata Sheria tutajiepusha na bugudha zisizo na maana, tutaepuka migogoro na polisi, tutapata fursa ya kushiriki kikamilifu katika kukuza kipato chetu na kuepuka utegemezi kiuchumi lakini muhimu zaidi tutaokoa maisha ya wasafirishaji na abiria wao.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawasihi waendesha pikipiki ambao wengi ni vijana kutambua kuwa maisha yao ni muhimu sana kwa Taifa letu. Nawaomba viongozi wa ngazi zote kuanzia Mitaa, Kata, Wilaya mpaka Taifa kuchukua hatua kupunguza vifo na walemavu wanaotokana na ajali za pikipiki katika maeneo yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa fursa hii naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana nakushukuru sana Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi. Kauli ya pili Mheshimiwa Naibu Waziri Mambo ya Ndani ya nchi.

Waheshimiwa Wabunge tuendelee kuvumilia kidogo kwa muda mfupi sana ujao.

## Mauaji Yanayofanywa na Askari Polisi

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 49 (1) ya Kanuni za kudumu za Bunge toleo la Aprili, 2013 naomba kuwasilisha ufanunuzi kuhusu kauli niliyoitoa nikijibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Rashid Ali Abdallah lililotokana na swali la msingi namba 290 tarehe 28 Mei, 2013 kwa kusema kuwa mauaji ambayo yanafanywa na askari polisi ni mauaji ya kisheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, tarehe 28 Mei, 2013 wakati wa kipindi cha maswali na majibu wakati nilipokuwa nikijibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Rashid Ali Abdallah lililotokana na swali la msingi Namba 290 la Mheshimiwa Khalifa Suleiman Khalifa, Mbunge wa Gando, kuhusu raia kuuwawa mikononi mwa Polisi, nilitumia maneno yafuatayo:-

*" Mauaji ambayo yanafanywa na askari ni mauaji ya Kisheria".*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa wa Kanuni ya 46 fasili ya kwanza ya kanuni za kudumu za Bunge toleo la Aprili, 2013 napenda kutoa ufafanuzi wa Kauli hiyo kufuatia muongozo wa Spika ulioombwa na Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, Mbunge wa Wawi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu cha 18 (a) cha Sheria ya kanuni ya Adhabu sura ya 16 kama ilivyofanyiwa mapitio mwaka 2002 kinampa haki mtu yoyote akiwemo askari kujilinda, kumlinda mtu mwingine, kulinda mali yake au mali ya mtu mwingine ikiwemo mali ya Serikali na taasisi zake ambayo iko chini ya uangalizi wake kisheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kutekeleza jukumu hilo kifungu cha 18 (b) na (c) cha Sheria hiyo kinatoa uwezo kisheria wa kutumia nguvu za kadiri hata ikibidi kiasi cha kusababisha madhara au kifo katika mazingira yanayoainishwa kisheria ambayo ni pamoja na haya yafuatayo:-

(a) Kuokoa uhai wake au uhai wa mtu mwingine;

(b) Kuzuia madhara makubwa ya mwili yasitokee kwake au kwa mtu mwingine;

(c) Kumzuia mtu anayetenda tendo ovu la kubaka au kunajisi mtoto au kufanya vitendo kinyume na maumbile; na

(d) Kumzuia mtu anayevunja nyumba usiku au unyang'anyi wa kutumia silaha au kuchoma nyumba moto au kufanya kitendo chochote kinachohatarisha uhai wa mtu au mali.

Mheshimiwa Naibu Spika, chini ya Sheria hiyo ya Kanuni ya Adhabu kifungu cha 77 na 78 kinabainisha kwamba askari Polisi, Hakimu au Afisa yoyote wa jeshi ambaye amekasimiwa mamlaka ya kuzuia au kutawanya maandamano yasiyo halali anaweza kutumia nguvu kutekeleza jukumu hilo na hata wajibishwa kisheria kwa kosa la jinai au madai kwa madhara yoyote yatakayotokea katika kutekeleza kihalali jukumu hilo.

Mheshimiwa Spika, aidha kifungu cha 21 cha Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai Sura Namba 20 kama ilivyofanyiwa mapitio mwaka 2002 kinampa mamlaka na kuweka mipaka ya matumizi ya nguvu katika kufanikisha ukamataji salama pasipo kusababisha madhara makubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kutafsiri Sheria, kanuni na taratibu mbalimbali nilizozitaja hapo juu Mahakama katika nyakati tofauti imetoa msimamo wa Kisheria juu ya suala hili. Mathalani kesi ya Seif Mohamed Senzagala dhidi ya Jamhuri ya mwaka 1994 kama ilivyonukuliwa kutoka *Tanzania Law Report* ukurasa 122 ambapo Mshtakiwa alimjeruhi kwa

panga mlalamikaji ambaye alimfuata nyumbani kwake na kuanza kumshambulia mahakama ya Rufaa pamoja na kuridhia uamuzi wa mahakama ya awali wa kumtia hatiani kwa kutumia nguvu kupita kiasi ilibainisha kuwa mshtakiwa hakustahili adhabu kubwa kwani alitenda kosa lile wakati akijihami *(self defence)* dhidi ya mashambulizi kutoka kwa mlalamikaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, ikumbwe pia kuwa kifungu cha 29 cha Sheria ya Jeshi la Polisi na Polisi wasaidizi sura ya 322 pamoja na kanuni za kudumu za utendaji wa jeshi la polisi *Police General Orders* Namba 274 vinampa haki ya kisheria askari polisi kubeba na kutumia silaha za moto zikiwemo bunduki na mabomu anapokuwa katika utekelezaji wa majukumu yake ya kila siku. Sheria na Kanuni hizo zimeweka masharti na utaratibu wa matumizi ya silaha hizo ambapo kila askari anayekabidhiwa silaha hizo anawajibika kwa matumizi yasiyo sahihi ya silaha alizokabidhiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kwa msingi huo tarehe 28 Mei, 2013 wakati nikijibu swali 290 nilitumia maneno mauaji yanayofanywa kisheria nikimaanisha mauji yanayotokea katika mazingira niliyoyaeleza hapo juu. Si nia ya Serikali kuhalalisha vitendo vya matumizi mabaya ya silaha ambavyo vinaweza kufanywa na askari wasio waadilifu kama ambavyo ilitafsiriwa na Mheshimiwa Mbunge. Serikali itaendelea kuhakikisha kuwa kila mmoja atatimiza wajibu wake kwa mujibu wa Sheria na yoyote atakayekiuka ajue Sheria ni msumeno.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuwahakikishia Waheshimiwa Wabunge kuwa jeshi la Polisi litaendelea kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa Sheria zilizotungwa na Bunge lako Tukufu pamoja na kanuni na taratibu zilizopo kwa weledi wa kutosha. Aidha kwa kuzingatia maelezo hayo jeshi la polisi limekuwa na litaendelea kuwachukulia hatua za kisheria na za kunidhamu askari wake wote watakaokiuka matumizi sahihi ya silaha wanazokabidhiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, jeshi la polisi litaendelea kuheshimu haki za raia na kujitahidi kutumia busara katika kutatua migogoro. Hata hivyo natoa tahadhari kuwa pale inapotokea kuwa migogoro inaelekea kuhatarisha usalama wa raia, amani na utulivu wa nchi. Jeshi la polisi halitakuwa na kigugumizi hata kidogo kutumia nguvu kurejesha usalama, utulivu na amani na hatimaye kuwafikisha wahusika mahakamani.

Mheshimiwa Naibu Spika, *Global Peace Index* ni kipimo kinachotumiwa ulimwenguni kiasi cha amani katika taifa. Katika mwaka wake wa saba sasa inapima na kuyapanga mataifa 162 kwa kuangalia viashiria chanya na hasi vya amani hususani uwepo wa vurugu au hofu ya vurugu katika nchi hizi. Kila nchi inapimwa kupewa alama kwa kutumia viashiria 22 vya amani ya ndani nchi ikiwemo kiasi cha uhalifu, idadi ya polisi kwa watu laki moja na kiasi cha *Organized Crimes.*

Mheshimiwa Naibu Spika, *Global Peace Index* ilianzishwa na *Institute for Economics and Peace* kwa waandalizi wa jukwaa la kujitegemea la wataalam kwa kutumia takwimu zilizokusanywa na kutolewa na taasisi ya *Economic Intelligence Unit.*

Taarifa na takwimu zinazotumika zinapatikana katika vyanzo vinavyoheshimika na kuaminika duniani kama *International Institute of Strategic Studies,* banki ya dunia, Mashirika mbalimbali ya Umoja wa Mataifa na taasisi zake, taasisi za amani na *Economic Intelligence Unit.*

Mhesheshimiwa Naibu Spika, kipimo hiki kinafanyika kwa kuangalia viashiria mbalimbali ikiwemo vigezo vya uwepo wa amani kama demokrasia, uwazi, elimu na ustawi wa taifa. *Global Peace Index* imekusudia kuchangia kwa kiasi kikubwa katika majadiliano kuhusu amani duniani na inaaminiwa na kutumiwa na mashirika mengi ya kimataifa, Serikali na Mashirika yasiyo ya Kiserikali ikiwemo Benki ya Dunia na umoja wa mataifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa taarifa ya hali ya amani duniani iliyotolewa na *Global Peace Index* mwaka huu amani duniani imepungua kwa asilimia tano katika kipindi cha miaka sita tangu 2008. Uhasama baina ya nchi umeendelea kupungua na kumekuwa na ongezeko kubwa la migogoro ya ndani ya nchi.

Nchi kumi zilizofanya vizuri zaidi kwa mwaka uliopita ni *Iceland, Denmark, New Zealeand, Austria, Switzerland, Japan, Finland, Canada, Sweden* na Ubelgiji. Wakati nchi zilizofanywa vibaya zaidi kwa ukosefu wa amani zimeongozwa na Afghastan iliyoshika namba 162 ikifuatiwa na Somalia, Syria, Iraq, Sudan, Pakistan, *DRC,* Urusi, Korea ya Kaskazini na Jamhuri ya Afrika ya Kati.

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi yetu imeendelea kushika nafasi ya 55 kama ilivyokuwa mwaka 2012 kwa kupata alama 1.89 takwimu hizi zinaonyesha kwamba Tanzania imeshika nafasi ya kwanza katika nchi za Afrika Mashariki na nchi inayotukaribia ni Uganda ambayo ipo nafasi ya 106. Watanzania tunao wajibu wa kulinda nafasi yetu katika jukwaa la Kimataifa kwa manufaa ya Taifa letu kiuchumi na kijamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ripoti hii nchi yetu imeendelea kuwekwa juu katika jukwaa la kimataifa kwa suala la amani. Bado nchi yetu inaendelea kuwa kisiwa cha amani pamoja na juhudi mbalimbali zinazofanywa na watu wasioitakia mema nchi hii kwa kusababisha vurugu kwa sababu mbalimbali zisizo na mashiko.

Watu hawa na mkakati wao wa kuichafua nchi yetu kimataifa hautafanikiwa kwa kuwa Serikali ipo makini na itaendelea kuchukua hatua madhubuti za kuimarisha usalama nchini na kuwalazimisha wote wasiopenda kufuata Sheria na kuzitii kwa lazima demokrasia isiyo na mipaka ni vurugu, uhuru pia usio na mipaka ni vurugu pia. Utamaduni wa kutoheshimu Sheria na taratibu unaendelea kujengeka nchini kwa kisingizio cha Demokrasia na kudai haki.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia nitumie fursa hii kuwaomba Waheshimiwa Wabunge na wananchi kwa ujumla kuheshimu na kufuata Sheria za nchi bila shuruti. Kuepuka kuweka mashindano ya kutotii Sheria na kulifanya jeshi la polisi ndiyo liwalazimishe kutii. Sote tukifuata sheria za nchi matukio ya vurugu na migogoro yatapungua sana nchini mwetu, hili linawezekana tukitimiza wajibu wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi nakushukuru sana. Mwongozo nilimwona Mheshimiwa Rajab. Miongozo miwili eeh, haya! Mwongozo pia, mitatu hiyo.

**MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMMED:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru, kwa kutumia Kanuni zetu za Bunge Ibara ya 68 (7). Wakati wa kipindi cha maswali na majibu hapa Bungeni leo wakati linajibiwa Swali Namba 458 lililoulizwa na Mheshimiwa Felister A. Bura, katika swali lake la nyongeza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Mheshimiwa Lukuvi katika majibu yake alisema kwamba Dodoma inapata fedha nyingi kuliko Halmashauri zozote hapa nchini na fedha zenyewe siyo zile fedha za madafu ni fedha za *World Bank.*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa uelewa wa wengi unaposema fedha za madafu maana yake ni fedha ambazo hazina thamani. Sasa kwa kuwa kauli hii na lugha hii imetoka kwa Waziri mzito, Waziri mwenye dhamana kubwa ina maana ni kauli ya Serikali. Tunaomba mwongozo wako fedha hizi za madafu nchini kwetu kulinganisha na Fedha za *World Bank* ni fedha za aina gani?

**MHE. HAROUB MUHAMMED SHAMSI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru nasimama mbele ya Bunge lako Tukufu kwa kanuni namba 68 (7) nakurejea na kanuni namba 63 (1) ambayo napenda ninukuu kanuni namba 63 (1) inasema:-

"Bila ya kuathiri masharti ya Ibara ya 100 ya Katiba yanayolinda na kuhifadhi uhuru wa mawazo na majadiliano katika Bunge ni marufuku kabisa kusema uongo Bungeni na kwa sababu hiyo Mbunge yoyote anapokuwa akisema Bungeni anawajibu wa kuhakikisha kwamba anatoa Kauli au maelezo kuhusu jambo au suala ambalo yeye mwenyewe anaamini kuwa ni la kweli na siyo jambo la kubuni au la kubahatisha tu".

Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa iliyotolewa na Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi sitaki kusema kama Mheshimiwa Waziri kasema uongo siwezi mimi kusema maneno haya kutokana na malezi niliyolelewa lakini ninachotaka kusema kwamba maelezo aliyoyatoa hayana ukweli na ni ya kubahatisha.

**NAIBU SPIKA:** Ziko mbili

**MHE. HAROUB MUHAMMED SHAMSI:** Ya Waziri wa Mambo ya Ndani.

**NAIBU SPIKA:** Kuhusu ajali za pikipiki?

**MHE. HAROUB MUHAMMED SHAMSI:** Sawa sawa naam.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika takwimu alizozionyesha katika kauli yake ukurasa wa pili anasema kwamba Mikoa inayoongoza kwa uwingi wa pikipiki kwa mujibu wa takwimu hizi ni jiji la Dar es Salaam yenye jumla ya pikipiki 2400. Akaendelea kusema kwamba katika idadi hiyo Wilaya ya Kinondoni ina jumla ya pikipiki 1735, Temeke ina pikipiki 1363 na Ilala ina pikipiki 1334.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukizijumlisha hizi unapata 4,432. Kwa hiyo, hoja yangu ni hapo nataka kupata Mwongozo wako juu ya ukweli wa takwimu hizi.

**NAIBU SPIKA:** Nakushukuru kwa umakini wako.

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru na mimi nataka kutumia kanuni ya 68 (8) utaniwia radhi kidogo kwa sababu la kwangu nilitaka kutoa taarifa lakini nisingeweza kumsimamisha Mheshimiwa Naibu Waziri wakati anajibu swali kwa hiyo nilisubiri mpaka nipate wakati muafaka.

Mheshimiwa Naibu Waziri Majaliwa Kassim Majaliwa alipokuwa anajibu Swali 459 lakini kufuatia swali la nyongeza la Mheshimiwa Dkt. Mary Mwanjelwa alirudia kauli ya kwamba Mbeya ni Manispaa karibu mara tatu, mara nne hivi, sasa hii inaweza ikawaaminisha Watanzania kwamba Mbeya ni Manispaa lakini wana Mbeya wenyewe watakuwa wanashangaa hivi tulishakuwa jiji miaka mingi iliyopita leo tumerudishwa kuwa manispaa. Kwa hiyo, nilitaka Mheshimiwa Naibu Waziri nimpe taarifa na Watanzania wengine wanaosikia kwamba Mbeya siyo Manispaa ni Jiji tena la siku nyingi sana. Hilo ndilo la kwangu.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana tunashukuru kwa hilo la mwisho umelimaliza wewe mwenyewe Mbeya ni Jiji kwa hiyo halihitaji maelezo mengine yoyote ya ziada. Tuanze na la pili kutoka mwisho Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, kama una la kusema kwa kifupi sana atafuata Mheshimiwa William Lukuvi.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nikiri nilishtuka sana Mheshimiwa Mbunge aliposema taarifa imejaa uwongo wa hali ya juu wakati ni wazi mtu yoyote makini anatambua kwa kweli hili ni kosa tu la uchapaji. Kwa hiyo kwanza kwa niaba ya Wizara yangu naomba radhi kwa kosa hili la uchapaji hii idadi ya pikipiki ni kama alivyonisaidia kuzijumlisha jumla yake ni 4,432.

Kwa hiyo, tutawaomba tu Waheshimiwa Wabunge wakati mwingine makosa ya namna hii jamani msitupige kwa lugha kali sana mnatushtua halafu tunadhani ni jambo kubwa kweli. Ahsante sana. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, URATIBU NA BUNGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu hoja ya Mheshimiwa Rajab, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, nilipokuwa najibu swali la Mheshimiwa Bura yeye alisema kwamba *CDA* pamoja na umuhimu wake imetengewa shilingi milioni 500 tu kwa ajili ya maendeleo. Mimi nikasema hapana siyo Shilingi milioni mia tano (500) tu imetengewa zaidi ya shilingi bilioni 32 hii ni tafsiri ya fedha za kigeni yaani imetengewa dola zenye thamani ya shilingi bilioni 32 na nikasema zaidi kwamba hizi fedha zimetokana na mkopo ambao Serikali imeingia kwa ajili ya kujenga miundombinu ya Dodoma.

Sasa kwa vyovyote vile kukopa *World Bank* ni *foreign money* ndiyo tafsiri yangu. Lakini niliposema shilingi 500 kwa tafsiri yake alisema shilingi milioni 500 ni lugha ya kawaida sijui kama mimi ni mtu wa kwanza kusikia pesa za madafu *(Tshs).*

Mheshimiwa Naibu Spika, tafsiri yangu ya lugha ya madafu nilikuwa narahisisha kumuambia kwamba hizi shilingi milioni 500 ni fedha za ndani, shilingi za Tanzania kama alivyosema yeye siyo hela ya madafu.

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Hata Nyerere alitumia.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, (SERA, URATIBU NA BUNGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, hela ya madafu ni lugha ambayo si rasmi sana lakini ni hela ya ndani huwa tunatumia lugha hiyo sana.

Kwa hiyo haina tafsiri tofauti na shilingi za Tanzania kwa hiyo nilichotaka kumthibitishia Mheshimiwa Bura ni kwamba milioni 500 zilizotengwa maendeleo ni fedha za ndani zinazotokana na kodi ya Watanzania lakini zile shilingi bilioni 32 ni thamani ya fedha za kigeni ambazo zimeletwa Dodoma kwa ajili ya kujenga miundombinu. Kwa hiyo 32 bilioni ni fedha za kigeni tafsiri yake lakini 500 ni shilingi za Tanzania.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri. Mambo haya ni sawa sawa tu na Mheshimiwa Chomboh alipokuwa anafafanua hapa na kutofautisha tofauti ya raha na starehe Kiswahili kigumu kidogo. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge niwashukuru sana bahati mbaya nilishasimama Mheshimiwa Kesy, bahati mbaya sana. Ungeniwahi ningekupa nafasi, tunakaribia mwisho wa mkutano wetu wa 11 ambao ulikuwa ni Bunge la Bajeti. Bado shughuli kubwa mbili tu, ambayo ni Muswada wa *Finance Bill* na Muswada wa *Appropriation.* Hiyo itashughulikiwa kadiri ambavyo mipango itakavyopangwa. Ndiyo maana mnaona kamati ya Bajeti wameshaondoka hapa wakifika mahali pazuri tunaweza tukashughulikia kesho au kesho kutwa kutegemeana na mrejesho tutakaopata kutoka kwa Kamati ya Bajeti, baada ya kuweka mambo yote sawasawa.

Naomba katika kumalizia shughuli hizi mbili Waheshimiwa Wabunge tuendelee kupeana ushirikiano ambao tumepeana tangu mwanzo ili kazi yetu iweze kukamilika. Kwa vile mkutano huu umekuwa ni mrefu sana na mimi baada ya hapa sitarudi tena kwenye kiti hiki, nichukue nafasi hii kuwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wote kwa ushirikiano mkubwa sana ambao mmetupatia uongozi wa Bunge katika kipindi chote cha Bunge hili la Bajeti, naomba niseme asanteni sana.

Tulipoanza tulikuwa kama tunapanda mlima lakini tumefika mahali mwisho vizuri tumeelewana, tumewafanyia Watanzania kazi njema sana. Kwa hiyo, nasema ahsanteni sana. *(Makofi)*

Lakini vile vile niseme ahsante sana kwa Wananchi wa Kongwa kwangu binafsi kwa kuniamini, kuendelea kuniamini na niwahakikishie kwamba baada tu ya Bunge hili nitarudi huko, nitapita kila mahali kuwachambulia jinsi Bajeti

hii ilivyo na maana kwao namna gani inatafsiriwa kwa maana ya maji, umeme, barabara, mishahara ya wafanyakazi na mambo yote safi kule Kongwa.

Kwa hiyo hilo wakae mkao wa kunisubiri niende nikawachambulie na naomba Wabunge na nyinyi muende kwenye majimbo yenu mkawaeleze Bajeti hii ina maana gani kwa wananchi msiendekeze huu upotoshwaji unaoendelea katika nchi wakati mambo mnayapanga nyinyi wenyewe halafu tena mnanyamazia. *(Makofi)*

Kwa hiyo, ni kazi ya kila Mbunge tukishatoka hapa kwenda kueleza kwa wananchi wake namna gani amefanikiwa kuwapenyezea maendeleo wananchi wake. Kama hakufanikiwa shauri yake. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge baada ya maneno hayo nimshukuru sana Mheshimiwa Spika, kiongozi wangu Anne Semamba Makinda, kwa uongozi wake imara na mahiri. Tunaendelea kumwombea. Kwa kweli amefanya kazi kubwa na ni matumaini yetu sote tunakubali kwamba kazi iliyofanyika ni kubwa sana na nzuri. *(Makofi)*

Baada ya maneno hayo kwa vile *Order Paper* ya leo imekamilika niwaombe Wajumbe ambao Kamati zenu mnaenda kukaa vikao hivi sasa, basi mkitoka hapa mwende moja kwa moja kwenye vikao vyenu. Kwa jinsi hiyo, basi naomba niahirishe shughuli za Bunge mpaka kesho saa tatu kamili asubuhi. *(Makofi)*

*(Saa 5.00 Asubuhi Bunge liliahirishwa Mpaka Siku ya Jumatano, tarehe 26 Juni, 2013)*